

SEPTEMBER - OKTOBER MMXXVI - TOLEO LA LIV

NGURUMO

ya Mwandishi



CHRISTINA
LUGOMERA

Ona Usikona

HABARI KUU:

"Bidhaisheni Kazi Zenu Ili Kulifikia Soko la Kimataifa"



Picha ya jalada: Christina Lugomera

HADITHI

SINDBAD BAHARIA—Uk 15

K.O.K.W.A—Uk 25 & 26

TUHUMA—Uk 27 – 28

DAWATI LA WATOZI

+255 766974865 -
WHATSAPP

+255 672 160 016
Piga

Richard Mwambe

YALIYOMO

MWANDISHI WETU

Jenipher Mkena

Uk 3

PITIO LA VITABU

DIWANI: CHUNGU TAMU—10

Uk 5

SAIKOLOJIA

Jibakishe Uwewe Wako...

Uk 5

Uk 6

MAKALA

Wajue Waandishi Wakubwa Afrika

Uk 7

Uk 8

KUTOKA KWA FANANI

Mti wa Faraja

Uk 9

SAKO KWA BAKO

Christina Lugomera

Uk 10

KUTANA NA MWANDISHI

Wilbard Makene

Uk 11

Uk 12

SHAJARA

Mjue Mtunzi

Uk 13

HABARI MOTO

Bidhaisheni Kazi Zenu kulifikia Soko...

Uk 16

SHUBAKA LA VITABU

Mjue Tawfiq Al Hakim (2)

Uk 17

KITABU NILICHOSOMA

Next Generation Leader

Uk 18

KUTOKA MAKTABA

William Shakespear

Uk 22

ELIMU JAMII

Safari ya Malezi 12

Uk 23

Uk 24

MWANDISHI WETU

Jenipher Alphonce Mkena

Katika toleo hili la 54, safu yetu imefika huko Ifakara. Katika mji huo tunakutana na mwandishi chipukizi Jenipher ambaye hakusita kuzungumza nasi kuhusiana na uandishi wake. Kuna uwezekano mkubwa kuwa hujawahi kumsikia au umewahi kumsikia. Basi Ngurumo ya Mwandishi inamleta kwako... msome umjue

Nimefurahi sana kuhojiana nawe maswali machache tu, ili msomaji wa jarida hili apate kufahamu. Tueleze kwa kifupi kuhusu wewe...

Jina langu ni Jennifer Alphonce Mkena. Nimezaliwa mwaka 1997. Ni mwalimu wa uchumi kitaaluma. Tokea nikiwa mdogo nilikuwa napenda sana kusoma hadithi na riwaya. Familia yangu pia ilipenda kusoma na walikuwa wafuatiliaji wakubwa wa riwaya za magazeti kama vile Sani, Kiu ya Jibu, Ijumaa na za vitabu.

Hawakuwahi kupitwa na toleo lolote kitu kilichofanya nipende sana sana ya uandishi.

Ilikuwa je ukapenda uandishi wa hadithi?

Nilipenda vile sana ya uandishi inaweza kuingia kwenye moyo wa mtu ikampa nafasi ya kuwaza juu ya wahusika na kutamani kuendelea kujua kuhusu nini kingempata mhusika. Nimeanza kuandika nikiwa shule ya msingi kwenye madaftari ambayo nilikuwa nawapa wanafunzi wenzangu wasome na nilikuwa napenda vile wanaponipa mrejesho na kufurahia hadithi zangu.

Waandishi wengi wa sasa upenda kutumia mitandao kama sehemu ya kujitambulisha kwa hadhira, vipi kuhusu wewe, umeshawahikuweka hadithi mtandaoni?

Hadithi yangu ya kwanza kuchapwa mtandaoni niliandika mara baada ya kuhitimu kidato cha sita. Baada ya hapo nimeandika hadithi takribani 10 na zipo nyinginge ambazo hazijakamilika.

Na vipi kuhusu changamoto unazokumbana nazo

Changamoto kubwa zinatoka ndani yangu mimi mwenyewe. Kuna wakati napoteza kabisa hamasa ya uandishi, najikuta nina mawazo mengi ya kuyaandika lakini nashindwa kwa sababu mbalimbali.

Kubwa kabisa kati ya yote ni muda na utulivu. Majukumu yamekuwa mengi kiasi nakosa muda wa kuandika na kumaliza. Nina hadithi nyingi ambazo bado hazijakamilika. Lakini kwa upande mwingine kuharibika kwa computer kumenifanya niwe mzito kumaliza kazi zangu.

Mimi bado sijachapa kitabu. Mpan-go wa kuchapa kitabu upo. Kwa sasa ninakazana nimalizie riwaya ninayoandika na mwaka 2027, panapo majaliwa nitachapa kitabu changu.

Je ni mwandishi yupi ndiye role model wako? (Awe wa nje au wa ndani)

Husein Issa Tuwa. Tuwa ni mwandishi mkongwe na mahiri

sana. Kila mara nnaposoma kazi zake nabakia na maswali mengi kwamba hivi huwa anawaza kwa namna gani mpaka anakuja na riwaya kama hii?!

Kuanzia wazo, mtiririko wa matukio, lugha ya uandishi na kila kitu kinakuwa kiko kamili kiasi msomaji lazima uhisi kuwa hili ni tukio la kweli limetokea mahali fulani, kwahiyo msomaji lazima ubebwe na hisia za kila namna kama ni huzuni ama furaha ama hasira kulin-gana na matukio.

Husein Tuwa anastahili heshima na kutambuliwa kimataifa kwa uandishi wake. Ninatamani siku moja riwaya zake zifanyiwe filamu na waigizaji mahiri na teknolojia ya kisasa. Nina imani zitasumbua sana kwenye ulimwengu wa filamu.

Sasa waeleze wasomaji, kama wanahitaji kukusoma, kazi zako zinapatikanaje?

Kazi zangu zinapatikana katika application ya hascavela lakini pia unaweza nami moja kwa moja kupitia namba **0756251987**

RM



KITABU KIPYA MJINI

Laura Pettie Amerudi Tena na ...

GARASA

Usiku mmoja, Gabi Kiza, msomi mlalahoi, analala akiwa na matumaini ya kuiona kesho yenye nafuu zaidi kuliko siku zote alizopata kuishi duniani. Aghalabu, nyumbani kwa Gabi panafukuta manyanyaso; huko nje nako ulimwengu unamsuta. Wanasema, *mwanaume asiye na kitu si mtu*.

Uchungu wa nafsi unamfanya Gabi aikubali ahadi ya Dunda. Ahadi ya kumwingiza *mchezoni* ili kuuvua umasikini uliomganda tangu utotoni. Huko *mchezoni*, Gabi anakutana na Ramona Bamsi, mwanamke mrembo mwenye pesa na ushawishi mkubwa

mitandaoni. Mambo yanachemka. Gabi anagundua ameruka jivu la umasikini na kuukanyaga motowa firauni.

Garasa ni riwaya ya kuisimua iliyosheheni visa, mikasa na taharuki; visasi, maumivu, machozi na damu. Ni riwaya inayokupa sura halisi za maisha, ambazo huenda hutapata kuziona mpaka pale utakapoingia *mchezoni* na kulamba garasa.

Kitabu hiki kinapatikana katika Duka la Vitabu la KONA YA RIWAYA, Kinondoni Morocco.

Kama upo mkoani na unakihitaji, piga simu 0655428085 utafikishiwa ulipo

Bei ni **15,000/=** tu


Nunua nakala yako ya GARASA kutoka moja kwa moja kwa Laura Pettie... upate yafutayo:-

- ♦ Kitabu kitasainiwa na mwandishi
- ♦ Kitabu chako kitagongwa Mhuri wa Moto wa rangi ya dhahabu
- ♦ Kitabu chako kitakuwa na QR Code ya shukrani kutoka kwa mwandishi.

Kumbuka:

- ♦ Kila shilingi 1,000 kutoka katika kila kitabu itachangia manunuzi ya mahitaji ya shule kwa watoto viziwi na wenye usikivu hafifu.

Hii ni kumuenzi mhusika mtoto mwenye ulemavu wa kusikia, ambaye yumo ndani ya riwaya hii.



PITIO LA VITABU

CHUNGU TAMU - 08

DIWANI YA CHUNGU TAMU

MWANDISHI: THEOBALD MVUNGI

WACHAPISHAJI: TPH

MWAKA: 1985

Inatoka toleo lililopita...

Mtindo

Mshairi ametumia mitindo yote miwili, yaani wa kimapokeo na wa kisasa.

Matumizi ya lugha

TAMATHALI ZA SEMI

- Tashibiha

Mweusi kama kiatu cha jeshi (Manzese mpa-
ka ostabei)

- Tashihisi

Katika ile baridi kali, mabomu ya mikono
yakatubusu miguuni (Daktari askari)

- Sitiari

Ushairi ni sukari tamu (Chungu tamu)

- Tafside

Nimekula naye tunda (Fikra za waungwana)

PICHA NA TASWIRA

Chatu – inawakilisha wanyonyaji

Kuku – wanyonywaji

Ngulu – vijiji/jamii iliyosahaulika katika ku-
patiwa maendeleo

MISEMO NAHAU NA METHALI

- Lakini haikutiwa chumvi mitaani

- Kuvaa masulupwete

- Umoja ni nguvu

- Sasa mwaleta shari

Kufaulu kwa mwandishi

Amejadili kwa kina matatizo mengi yanayozipata jamii za kiafrika, pia amejaribu kutoa masuluhisho ya matatizo hayo.

Vilevile amefaulu kutumia mitindo yote miwili, kimapokeo na kisasa.

Kutofaulu kwa mwandishi

Baadhi ya mashairi yametumia lugha ngumu ambayo inamfanya kila mhakiki alifasiri shairi kwa mtazamo wake.

MWISHO


TAMU NA CHUNGU

Sikiliza nikwambie, upate kutambua
Maisha tunayoishi, yana mambo ya ajabu,
Kuna raha na furaha, na shida za kusumbua,
Ukiyaona ya leo, kesho hutoyatambua.

Kuna wakati wa kiceko, na furaha kupitiliza
Kila jambo likinyooka, bila hata ya vikwazo
Ndiyo utu uzuri wake, amani inayotawala
Tamu ya haya maisha, kila mtu huipenda.

Lakini punde si punde, mawingu yakitanda
Uchungu ukija juu, mahangaiko yakawa
Usiache kutumaini, maisha ni mzunguko
Chungu ikiisha leo, kesho tamu itarudi

Daima kumbuka moyoni, vumilia kila hali
Chungu na tamu pamoja, ndiyo msingi wa maisha
Ukipata ya furaha, shukuru uwe na amani
Ukiyapata machungu, jipe moyo utasonga





SAIKOLOJIA

Na: NEEMA MGAO

MALKIA WA SAIKOLOJIA

+255763013206

JIBAKISHIE UWEWE WAKO KATIKATI YA MISUKOSUKO

Ni mwezi wa kumi [10] sasa tumefika, tunaelekea kuumaliza mwaka huu wa 2026. Mwaka ambao pengine umeenda tofauti na ulivyopanga iwe, mwaka ambao pengine mambo yamekuendea vizuri sana zaidi ya matarajio yako. Shukuru Mungu kwa yote. Endelea kuwa imara. Kwakuwa bado unapumua na kuishi, panga tena na tena mipango yote iliyokuendea arijojo ili uibunie mbinu mpya za kuitekeleza mipango hiyo. Na Mungu akutangulie.

Katika uwanja huu wa SAIKOLOJIA ndani ya toleo hili, tuangazie mada isemayo JIBAKISHIE UWEWE WAKO KATIKATI YA MISUKOSUKO.

Maisha ya binadamu yanaundwa na nyakati kuu tatu, nazo ni..

1. Wakati wa furaha

Huu ni wakati ambao kila kitu mtu lichopanga chaweza kuwa kinaenda vizuri, au ni wakati ambao mambo yamemnyookea. Huu ni wakati anaofurahia mafanikio katika maisha yake. Ni wakati awapo kwenye kilele cha mafanikio au anaelekea kilele cha mafanikio.

2. Wakati wa huzuni / masikitiko

Huu ni wakati ambao mambo ambayo mtu aliyapanaga yamemwendea vibaya au yamemwendea tofauti. Yaweza kuwa biashara haziendi, ndoa inamsumbua au yupo kwenye changamoto ya maradhi. Yaweza kuwa ni nyakati za msiba au maumivu kwake.

3. Wakati wa katikati / asiojielewa

Kuna wakati wa kutokujielewa, yaani kunakucha au unashinda ukiwa hujielewa kuwa uko na furaha au uko na huzuni, wamerahisisha wameita *"nipo nipo tuu"*. Huu ni wakati ambao mtu hushindwa ku-

jitambua kuwa yupo na furaha au yupo na huzuni.

Katika nyakati hizo zote, nyakati ngumu ni nyakati uwapo kwenye matatizo au misukosuko, huu ndiyo wakati nilioona leo tuangazie kidogo kutokana na wengi kushindwa kuumudu wakati huu.

Unapokua na matatizo, unapokumbwa na mtihani wa maisha, iwe umefukuzwa kazi, iwe umefiwa, iwe umekumbwa na maradhi, iwe unauguliwa na mpendwa wako ni wazi kuwa utakuwa umevurugwa kiufahamu, haijawahi kutokea, kwamba uwe katikati ya matatizo kisha uwe unajikumbuka hata kuoga au kwamba uwe katikati ya matatizo kisha ufurahie, yaani uwe kawaida, shetani huyo hajazaliwa na sidhani kama ameumbwa teyari. Matatizo yanapomkumba binadamu ni wazi kuwa asipopata msaada wa mtu wa karibu wa kumsimamia na kuambatana naye ni wazi kuwa anaweza hata asioge hata wiki na zaidi. Matatizo au misukosuo huuondoa utu wa mtu husika.

JIBAKISHIE UWEWE WAKO KATIKATI YA MISUKOSUKO

Kujibakishia uwewe wako katikati ya misukosuko ni hali ya kujikumbuka na kujitunzia ubinadamu na utu wako kama si jinsia yako katikati ya misukosuko.

Ni ile hali ya kujikumbusha kuwa wewe ni nani na inapaswa uweje,

Ikiwa ni mwanaume, ni ile hali ya kujikumbusha kuwa hata kama unapitia jambo gani, mindhari wewe ni mwanaume inakubidi uwe imara zaidi ya nyakati zote.

Ikiwa ni mwanamke, ni ile hali ya kujikumbusha kuwa hata kama unapitia jambo gani, usiache kudeka na kuoonyesha kuwa vyovyote iwavyo wewe ni mwanamke inapaswa uwe safi na unukie kikike.

Unapitia madhila sawa, jibakishie huo utu wako, usijimalize kiasi cha kujisahau kama wewe ni nani hata uwe unapitia nini.

SAIKOLOJIA

Chochote unachopitia, usisahau kuwa wewe ni binadamu, umeumbwa na unaishi kwa kusudi la Mungu wako unayemwamini hivyo kujifurahia na kujikumbusha u-wewe wako ni muhimu sana. Maisha ni pumzi. Maisha yako yanakutegemea wewe mwenyewe. Maisha na usalama wako ni wewe kwanza wa kujitazama na kisha ndipo wengine wakutazame na wewe utazame wengine. Ni ngumu sana kwa mama unaye-*swampa* kutwa kucha kila kona upo wewe tuu, hata kunawa uso tu hunawi, unaramba kidole na kukitia kwenye kona za macho kutoa tu tongotongo za usiku, eti kunakucha kuchakarika mchakariko uliokutoa kwenye uanamke wako, wewe ni ngumu kumfundisha huyo mwanao kuwa kuna kitu kinaitwa usafi au kuoga, HUTOWEZA.

Jikumbuke, jibakishie u-wewe wako, jibakishie huo utafauti wako na wangu, wewe huwezi kuwa mimi, ni sahihi, ni kweli sijui unachopitia, sijakataa, lakini nionyeshe mimi huyo mtu aliyeshinda mtihani kwa yeye kujisahau. Kwamba alipata kazi kwa yeye kuacha kuoga, kwamba aliponyesha mgonjwa wake kwa yeye kuacha kula. Nimuone huyo mtu aliyefanikiwa kuitunza familia na kufanikiwa kulea vizuri watu wa nyumbani kwake kwa yeye kujifungia ndani kwamba ye hajielewi elewi yaani. NI WAZI KUWA HAYUPO.

Kuanzia leo unaposoma makala hii, niahidi kuwa hau-tojisahau tena, Niahidi kuwa utautunza u-wewe wako, Niahidi kuwa utakuwa imara nyakati zote ili jamii ikuzungukayo iwe imara pia.

Zipo njia kadhaa ambazo zitakufanya ujibakishie u-wewe wako katikati ya nyakati za misuko suko.

Weka majadiliano mafupi na wewe wa ndani. Kuna kujisahau, ila hakikisha unapata muda wa walau dakika moja tu, popote pale utapokuwapo, hata chooni, ila pata muda wa kujadiliana na nafsi yako ili-yopo ndani mwako. Mjadala uhusiane na mwenendo wa mambo ulivyo, kwamba jambo lilianzaje, limefikia wapi, na litakuwaje. Ukiona hayaeleweki yaache yaende vile Mungu atakavyoyapeleka. YASIKUCHOSHE.

Hakikisha unaye mtu wa kukwambia ukweli. Maisha yanahitaji watu, katika hatua ya kuhakikisha unajibakisha mwenyewe, uwe na mtu mmoja ambaye akisema jambo unamsikiliza, uwe na mtu wa kukwambia ukweli na wewe ukajiambia "ILA KWELP". Uwe na mtu wa kukutazama na kukusaidia, ukikosa

mtu huyo, wewe na Mungu msipishane mahali popote, mwende sambamba.

Sikiliza sauti ya ndani.

Hapa inaweza kuwa sauti yako binafsi baada ya majadiliano, au yaweza kuwa ni sauti ya Muumba ndani yako ambayo ndiyo itakayokufungia mjadala wa hoja tatizika. JISIKILIZE.

Tunapoelekea kumaliza mwaka nimeonelea tuangazie mada hii ili itufae sote. Nakutakia maandalizi mema ya kufungia mwaka.

Kwa huduma ya ushauri wa kisaikolojia kuhusiana na Mapenzi, ndoa, mahusiano, malezi ya watoto wa kufikia, malezi ya watoto wa kuwazaa, malezi ya vijana na mambo yote yahasuyo maisha usisite kuwasiliana name kupitia +255763013206 ili nikupatie huduma hiyo.

KARIBU SANA.

MADAM NEEMA MGAO.

QUEEN OF PSYCHOLOGY.

DODOMA.

TANZANIA.



MEROME
COMPANY LIMITED
"Your Vision, Our Mission"

HUDUMA ZETU

- PRINTING
- PPE
- SUPPLY OF STATIONARY
- SUPPLY OF BUILDING MATERIAL
- SUPPLY OF ICT AND TEHAMA
- PROMOTION ITEMS
- CCTV CAMERA

+255712345316
meromecompany@gmail.com
Dar es salaam
Tanzania

WAANDISHI WAKUBWA WA FASIHI AFRIKA

TAFAKURI YA MWANASESEME

WAANDISHI 7 WAKUBWA ZAIDI WA FASIHI BARANI AFRIKA.

Na Mkuluwanyika.

Afrika imetoa magwiji wa fasihi ambao maandiko yao yamevuka mipaka, yakapinga utawala wa mabavu, yakalinda kumbukumbu za kihistoria, na kubadilisha jinsi ulimwengu unavyoielewa Afrika.

Chini kunaorodha ya waandishi saba wakubwa zaidi wa fasihi barani Afrika. Katika mpangilio wa orodha hii, tuliangalia zaidi ya Tuzo za Nobel na umaarufu wa kawaida. Waandishi hawa walilinganishwa kwa kutumia vigezo saba: ukubwa wa kazi zao za kifasihi, mchango wao katika fasihi ya Afrika, tuzo na heshima kubwa walizopata, ushawishi wao duniani, mafanikio ya kitalaam na kifikra, athari zao kihistoria na kitamaduni, pamoja na kudumu kwa urithi wao.

NAMBA 1 — WOLE SOYINKA

Mwandishi wa michezo ya kuigiza, mashairi, riwaya, insha, mchambuzi wa fasihi na mwanafikra wa kisiasa ambaye kazi zake zimegusa karibu kila nyanja kuu ya uandishi.

Kazi zake maarufu ni pamoja na *Death and the King's Horseman*, *The Man Died*, *The Interpreters*, na *A Dance of the Forests*.

Mnamo mwaka 1986, Soyinka alikuwa Mwafrika wa kwanza kushinda Tuzo ya Nobel ya Fasihi.

Lakini umuhimu wake unazidi tuzo hiyo. Alisaidia kujenga sanaa ya jukwaani ya kisasa barani Afrika, akapinga uonevu wa kisiasa kupitia maandiko yake, na kuleta utamaduni wa Kiyoruba katika taaluma ya fasihi ya kimataifa.

Kwa nini yuko #1: Uwezo mkubwa katika aina mbalimbali za uandishi, ushawishi mkubwa barani Afrika, utambulisho mkubwa duniani, na urithi unaovuka sanaa moja pekee.

NAMBA 2 — CHINUA ACHEBE

Ni waandishi wachache sana wa Afrika waliobadilisha taswira ya Afrika duniani kupitia fasihi kama Chinua Achebe.

Riwaya yake ya mwaka 1958, *Things Fall Apart* (Shujaa Okonkwo), imekuwa moja kati ya riwaya za Afrika zilizosomwa zaidi na kutafsiriwa katika lugha zaidi ya 50.

Kazi zake zingine kuu ni *No Longer at Ease*, *Arrow of God*, *A Man of the People*, na *Anthills of the Savannah*.

Achebe pia alikuwa mhariri, mwandishi wa insha, mchapishaji, na mchambuzi wa fasihi aliyesaidia kukuza vizazi vingi vya waandishi wa Afrika.

Kwa nini yuko #2: Ushawishi wake katika fasihi ya Afrika ni mkubwa mno. Hakuandika tu kuhusu Afrika, alisaidia kubadilisha nani mwenye mamlaka ya kusimulia hadithi ya Afrika.

NAMBA 3 — NAGUIB MAHFOUZ EGYPT

Msimulizi mkuu wa maisha ya mji wa Cairo.

Mahfouz aliandika zaidi ya riwaya 30 na mamia ya hadithi fupi, huku maandiko yake yakigusa jamii ya Misri, familia, siasa, imani, maisha ya kisasa, na maisha ya kila siku.

Kazi yake bora zaidi, *The Cairo Trilogy*, ilikuwa nguzo kuu ya fasihi ya kisasa ya Kiarabu.

Mnamo mwaka 1988, alikuwa mwandishi wa kwanza wa lugha ya Kiarabu kupokea Tuzo ya Nobel ya Fasihi.

Kwa nini yuko #3: Wigi wa kazi zake za fasihi, ushawishi wa kimataifa, ushindi wa Tuzo ya Nobel, na mchango wake wa mabadiliko katika fasihi ya Kiarabu.

NAMBA 4 — NGŪGĨ WA THIONG'O

Ngũgĩ hakuwa mwandishi wa riwaya tu. Alikuwa mmoja wa sauti zenye nguvu zaidi barani Afrika kuhusu lugha, ukoloni, na uhuru wa kitamaduni.

Kazi zake kuu ni pamoja na *Weep Not, Child*, *A*

MAKALA

Grain of Wheat, Petals of Blood, Devil on the Cross, Matigari, na Wizard of the Crow.

Kitabu chake chenye ushawishi mkubwa, Decolonising the Mind, kilikuwa hoja kuu iliyowahimiza waandishi wa Afrika kutumia lugha zao za asili na mtazamo wa kitamaduni wa Afrika.

Msimamo wake ulikuwa na gharama: maandiko yake na sanaa ya jukwaani iliyogusa siasa vilimsababishia kifunyo nchini Kenya na hatimaye kuishi ukimbizini.

Kwa nini yuko #4: Ushawishi mkubwa wa kifasihi barani Afrika, umuhimu wake kifikra, na urithi unaovuka riwaya hadi kwenye mijadala mipana ya kujitenga na fikra za kikoloni.

NAMBA 5 — NADINE GORDIMER

Gordimer alitumia fasihi kukabiliana changamoto ya kisiasa ya karne ya 20 katika nchi ya Afrika kusini (ubaguzi wa rangi).

Kazi zake kuu ni The Conservationist, Burger's Daughter, July's People, na A Sport of Nature.

Vitabu vyake kadhaa vilipigwa marufuku na serikali ya ubaguzi wa rangi.

Mnamo mwaka 1974, alishinda Tuzo ya Booker, na mwaka 1991 alipokea Tuzo ya Nobel ya Fasihi.

Kwa nini yuko #5: Mchango mkubwa wa kihistoria na kitamaduni uliunganishwa na mafanikio makubwa ya kifasihi na kutambulika kimataifa.

NAMBA 6 — MIA COUTO

Mia Couto anawakilisha upande mwingine muhimu wa fasihi ya Afrika: Afrika inayozungumza Kireno (Lusophone Africa).

Mwandishi huyu wa Msumbiji ameandika riwaya, hadithi fupi, na mashairi yanayochanganya lugha ya Kireno na lugha za Msumbiji, mila, ngano, na mtazamo wa ulimwengu.

Riwaya yake maarufu, Sleepwalking Land, ilikuwa kazi bora ya fasihi iliyotambulika kimataifa.

Couto amepokea tuzo muhimu zaidi za fasihi katika ulimwengu wa Kireno, ikiwa ni pamoja na Tuzo ya Camões na Tuzo ya Kimataifa ya Fasihi ya Neustadt.

Kwa nini yuko #6: Sauti ya kipekee ya kifasihi iliyobadilisha uandishi wa Afrika kwa lugha ya Kireno huku ikiwafikia wasomaji mbali zaidi ya Msumbiji.


NAMBA 7 — J. M. COETZEE

Coetzee alikuwa mmoja wa waandishi wa riwaya muhimu zaidi waliotoka Afrika Kusini.

Kazi zake kuu ni Waiting for the Barbarians, Life & Times of Michael K, Disgrace, na Elizabeth Costello.

Alishinda Tuzo ya Booker mara mbili — kwa Life & Times of Michael K (1983) na Disgrace (1999).

Inaendeeza Ukurasa wa 34 ➡



KUTOKA KWA FANANI

REBECCA KITOMARI

MTI WA FARAJA ULIFIKA SHULE YA SEKONDARI KITEFU—ARUSHA

Tarehe 24/9/2026 nilipata fursa ya kipekee kama Mkurugenzi wa Disaster Education and Resilience Initiative (DERI) kushiriki katika hatua muhimu ya kujenga jamii yenye uelewa, maandalizi na ustahimilivu dhidi ya majanga na changamoto za mabadiliko ya tabianchi.

DERI ni shirikika lisilo la kiserikali (NGO) linalojishughulisha na elimu ya majanga na mabadiliko ya tabia nchi kama zana muhimu katika kujenga jamii salama.

Kupitia Mradi wa Mti wa Faraja, tulikutana na wanafunzi na walimu ambapo tulifanya shughuli mbalimbali zikiwemo:

1. Kutoa elimu kuhusu mabadiliko ya tabianchi na athari zake, Kujifunza kuhusu majanga, maandalizi na namna ya kupunguza madhara, ikiwemo changamoto zinazoweza kuhusishwa na mvua kubwa za El Niño.
2. Kuwatambulisha wanafunzi kitabu cha Mti wa Faraja kama nyenzo ya kujifunza na kuchukua hatua

3. Kuanzisha/kuimarisha Environmental Safety Club kama jukwaa la wanafunzi kujifunza na kuchukua hatua kuhusu mazingira

4. Kufanya zoezi la upandaji wa miti, huku wanafunzi wa Kidato cha Kwanza wakipewa jukumu la kuwa walezi na wafuatiliaji wa miti hiyo katika safari yao ya miaka 4 shuleni.

Tunataka kuona wanafunzi wakipata uelewa wa namna ya kujiandaa kabla ya majanga, wakati wa majanga na baada ya majanga.

Nawashukuru sana uongozi, walimu na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kitefu kwa kutupokea na ku-shirikiana nasi katika hatua hii muhimu.

Pia ninawapongeza timu ya DERI na wadau wote wanaoendelea kuamini katika maono yetu ya kujenga jamii salama, imara na yenye ustahimilivu.

Naomba mfuatilie kurasa zetu:

Instagram: @deritanzania

Facebook: deritanzania



Rebecca Kitomari (wa pili kutoka kushoto), mwandishi wa kitabu cha Mti wa Faraja akiwa katika picha ya pamoja na wanachama wa DERI (Disaster Education and Resilience Initiative) katika moja ya kampeni zao za kupambana na mabadiliko ya tabia nchi.

Kutoka Orchid Café, Dar es salaam...

Mazungumzo yangu na Bi. Christina Charles LUGOMERA yalifanyika katika mgahawa wa Orchid jijini Dar es salaam alipoleta kitabu chake cha MPATANISHI ili kipate saina ya mtunzi. Sikupenda kuiacha fursa hii na moja kwa moja tuli- zungumza kuhusu usomaji wa vitabu kwake.

Kusoma vitabua au tuseme kupenda kusoma kulianzaje ndani yako?

Nikiwa *Nursery* nilikuwa nachekwa sana na watoto wenzangu kwa mambo mawili; sijui kusoma kama wao na sijui kuandika namba 4. nakumbuka niliwashitaki kwa mama yangu. Mama akaniambia “Jifunze kusoma na kuandika uwazidi wote. Kila sehemu, kila siku unapopita ukiona maandishi, soma, hata namba zitamke, utajua. Na kila niliposoma alinipongeaza na kuniambia “Unjaua kuliko wao”. Hii ilinipa motisha ya kupenda kusoma.

Aina gani ya maandiko unayopenda kusoma?

Mimi nasoma kila kitu, lakini zaidi vitabu na machapisho kadhaa ya mitandaoni kwa watu wanaonigusa. Pamoja na kwamba napenda kusoma, lakini sismi kila kitu kama zamani. Mama yangu aliniambia nisisome kila kitu baada ya kunikuta na kipande cha karatasi kinachoeleza maelekezo na matumizi ya mipira ya kiume name nilikuwa bado mdogo sielewi kitu (akacheka). Vitabu zaidi kwa sababu ndani ya vitabu kuna utulivu, ukimya na maarifa mengi sana.

Kwasasa bado ari ya usoaji wako inaendelea au imepungua kutokana na majukumu?

Ndiyo. Kadiri umri wangu unavyoongezeka natamani ningejua thamani ya vitabu kwa ninayoyapenda tokea zamani. Mwanzoni nilikuwa nasoma kila kitu, kumbe nilipaswa kuchagua kwa ustawi wangu. Huenda ningetambua usomaji wa vitabu nikiwa mdogo, ningehamasisha watoto wengi sana. Kwa kifupi ari ya usomaji kwangu inaongezeka kila siku.

Ok! Kuna mengi ya kujifunza kutoka kwako... unawaambia nini wale wasiopenda kusoma vitabu?

Vitabu vinajenga. Vinaitengeneza akili, mimi vitabu huniponya. Kuna time nakuwa nimevurugwa, macho yangu yakitua kwenye kitabu natulia.

Kwa ambaye si mpenzi au mvivu wa kusoma vitabu... namshauri ajaribu kidogokidogo. Kila mahali unapoenda weka kitabu kwenye bag yako, fanya kama nauli. Kitabu kisikae mbali na wewe, na ukianza kusoma faida yake utaiona.

Mwandishi gani hapa Tanzania anakuvutia kwa kazi zake?

Kwa hapa Tanzania mwandishi anayenivutia ni Beka Mfaume, wewe mwenyewe Amata na ndiyomaana nipo hapa, Hayati Shaaban Robert na mwanamama Laura Pettie.

Lakini pia navutiwa na maandiko ya mtandaoni hasa ya Masoud Kipanya na huyu Florine Willy.

Shukrani kwa Bi. Christina, naamini kutoka kwake kuna ulilojifunza. Basi tuendeleo kusoma Ngurumo ya Mwandishi ili tujifunze zaidi.

Katika toleo lijalo, nani atakuwa kwenye Sako kwa Bako?

Pichani: Christina Lugomera



KUTANA NA MWANDISHI WILBARD MAKENE

Na Mwandishi wetu

Katika safu yetu hii ya Kutana na Mwandishi, leo tupo mezani na Wilbard Makene. Wilbard Makene si jina geni masikioni mwa wapenzi wa riwaya za Kijasusi.

Wilbard Makene anayetamba na riwaya zake kama Sara-fu ya Gavana, Uchochoro wa Tanzanite, Ufafanuzi Lu-galo na nyinginezo, leo anatusimulia safari yake ya uandishi...

Bwana Wilbard, hebu tueleze kuhusu wewe...

Mimi ni mtoto wa kwanza katika familia ya watoto watano. Mzazi wa kwanza alifariki nikiwa darasa la nne, na mwingine alifariki mwaka mmoja baadae. Nimelelewa na kuku-kulia kwa mjomba mpaka kufika kidato cha sita. Baadae nilihamia Dar es salaam kwa Mama Mkubwa ambako nilimaliza na kupata Shaha-da ya Kwanza ya Utunzaji Mazingi-ra na Viumbe Maji Mwaka 2008 kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Sa-laam.

Serikali ilinipangia kwenda kufanya kazi ya ualimu, sikwenda, nilitaka kufanya kazi niliyosomea; na katika sekta binafsi. Sikupata kazi, na ilibidi kuanza kujitolea kwenye ma-shirika bila malipo. Nilipata kazi kama mkusanyaji na mchakata takwimu baada ya mwaka na nusu wa kujitolea.

Safari yangu ya kufanya kazi kwenye taasisi binafsi za uhifadhi mazingira na ukuzaji viumbe maji ilianza rasmi.

Na vipi kuhusu safari yako ya kiuandishi?

Nilianza kuandika mwaka 2018 baada ya kusoma vitabu cha Robert Kiyosaki, The Quadrant Cashflow. Nilijiona mjinga na ninayeelekea kwenye lindi la umaskini baada ya kusoma.

Kuanza kuandika ilikuwa kama se-hemu yangu ya: kufanya ubongo wangu kufikiri na kuwa mtaji;

kukataa ubongo wangu kulala—nilijua kuwa ili niwe mwandishi mzuri, ilinibidi nisome sana; kutoa sehemu ya mchango wangu kuelimisha jamii ya sasa na vizazi vijavyo. Nilipenda jinsi Robert Ki-yosaki alivyotumia lugha nyepesi kuelezea jinsi wengi wetu tulivyo mbumbumbu kwenye utafutaji, ukuzaji mtaji na hata matumizi.

Je uandishi wa Riwaya ndiyo ka-zi unayoitegemea katika mai-sha?

Hapana. Baada ya kufanya kazi kwa miaka nane na kupata uzoefu kazini nilijiajiri kama Mshauri Mwelekezi wa Uchumi wa Buluu hasa eneo la utunzaji mazingira viumbe maji, mazingira yake, na uvuvi. Mimi ni mfanyabiashara; na muwekezaji pia.

Wewe kama mwandishi mkubwa na makini, je ni changamoto ga-ni umepambana nazo katika sa-fari yako ya uandishi na umezi-vukaje?

Changamoto kubwa ilikuwa kumpata mchapishaji atakayekubali kuchapisha, kuzindua, kusambaza, na kutoa mrabaha kwa jinsi nayoona inafaa. Ili kufanikisha hili na kuepuka hadaa, ilinibidi kufanya kazi zote mwenyewe na kwa pesa zangu kwanza—ambako nilikumba-na na baadhi ya matapeli. Baada ya kujua jinsi tasnia na wadau wake inavyofanya kazi, nilipata sehemu kubwa ya



WILBARD MAKENE

Mmoja wa waandishi mahiri wa hadithi za kulisimua nchini Tanzania

suluhisho baada ya kupata kampuni ya kusimamia kazi zangu huku ni-kiendelea na majukumu mengine.

Kwa Sasa jina "Wilbard Makene" ni jina linalotajwatajwa sana kwenye midomo ya wapenda fasihi. Hebu tueleze, unafikiri siku Moja UANDISHI utakule-tea heshima fulani mbele ya ja-mii?

Siwezi kusema moja kwa moja kuwa nina ndoto za fasihi kuniletea heshima kubwa kwasababu jukumu hili ni la wasomaji. Ninachoweza kusema ni kwamba, nitaendelea kuandika kwa weledi na mapenzi, maana kwangu uandishi ni kazi ili-yotukuka. Ni kazi takatifu. Fedha zinazopatikana ni sehemu ndogo ya picha kubwa ya manufaa ya uandishi kwenye jamii.

Sasa hebu tuitazame kalamu yako. Kati ya Simulizi zako ulizo-

KUTANA NA MWANDISHI WILBARD MAKENE

andika, ni ipi imependwa sana na hadhira kadiri ya mirejesho unayopokea. Na Unafikiri Kwa nini?

Sina jibu la moja kwa moja, ila itoshe kueleza kuwa mapokeo ya kazi zangu yanategemea fani na haiba ya aliyepokea kazi na jinsi kitabu kinavyoakisi eneo lake la kazi. Mfano, Uchochoro wa Tanzanite kimepata sifa nyingi maeneo ya Moshi na Arusha — Tanzanite inakopatikana. Mkwe wa Jaji Mkuu imependwa Mahakamani na kwa wapenzi wa riwaya za mapenzi. Ufafanuzi Lugano kimeshabikiwa na wanajeshi, wakati Uozo Bandarini imetamba kwa maofisa wa bandarini na maeneo ya mipakani. Sarafu ya Gavana, Kifurushi Ikulu, Kabrasha la Rais, na Mkono wa Jamhuri navyo vina wapenzi wasiopenda kusema hadharani.

Mpaka Sasa umeshachapa vitabu vingapi? Na katika hivyo ulivyochapa ni kipi ambacho wewe mwenyewe ukikitazama na kukisoma unasema "Naam hapa niliandika"?

Jumla ni vitabu 10, nane viko sokoni, viwili viko kwa mchapishaji—APE. Vitabu nane vilivyochapishwa—Sarafu ya Gavana, Kifurushi Ikulu, Kabrasha la Rais, Mkono wa Jamhuri, Uchochoro wa Tanzanite, Ufafanuzi Lugalo, Uozo Bandarini, na Mkwe wa Jaji Mkuu.

Kuhusu kitabu nachopenda: vitabu vyote ni vizuri na vyenye vionjo vya kipekee—kila kimoja kwa namna yake. Kila kitabu kina nafasi yake katika moyo wangu, kimebeba kumbukumbu muhimu wakati kikiandikwa, mafunzo kiliyonipa na namna kilivyopokelewa sokoni. Kila kitabu kimekuwa ngazi muhimu kwangu kuendelea kunifanya nipende kuandika zaidi.

Bwana. Makene, una mke na watoto? Kama ndiyo, hebu Tueleze ushiriki wao katika uandishi wako. Maana nasikia waandishi ni watu *bize* mpaka hawana muda na wenzi wao. Hebu tueleze Kwa upande wako, mambo yanaendaje huko?

Nina mke na watoto watatu. Mimi huandika asubuhi, kati ya saa kumi na mbili mpaka saa tatu asubuhi kabla sijaanza kazi nyingine binafsi. Akili yangu huwa imetulia na mke hushiriki kwa kuniandalia kifungua kinywa; na kuhakikisha hakuna kelele eneo nalokuwa nimekaa. Napewa ushirikiano mzuri sana kwenye kazi zangu za fasihi.

Nimepita katika maduka ya vitabu, naweza kusema kwamba vitabu vyako karibu vyote nimevikuta kwenye maduka ya Elite. Unaweza kutupa siri ya jinsi Gani umepenya huko? Na je kama mwandishi

unaonaje faida ya kufanya kazi na publisher mkubwa kama APE?

Elite ni kampuni ya usambazaji na mauzo ya kampuni ya uchapishaji—APE. Hawa ni wachapishaji wa pekee na wasambazaji ambao kwa haiba ya utendaji, nilijua watanifaa kulingana na mazingira ya sasa ya uchapishaji nchini.

Ili kuweza kufanya nao kazi, ilinibidi kwanza kuchapisha mwenyewe ili kulifahamu soko vyema. Baada ya hapo niliwatafuta nikiwa tayari nafahamu kilichoko sokoni ili niweze kuwa na uwezo wa kutengeneza mazingira ya mikataba yenye ushindani.

Faida kubwa ya kufanya kazi na APE ni kwamba ninaweza kufanya kazi zangu nyingine za kujiingizia kipato huku APE wakiendelea kusimamia kazi zangu za uandishi. Hata hivyo, APE hushirikiana na makampuni mengine kama Mkuki na Nyota katika usambazaji wa kazi zangu—nashukuru Mungu.

Na Kwa kumalizia, je unafikiri nini au una lolote ambalo umefikiri kuwasaidia waandishi chipukizi kukua katika tasnia hii?

Kipindi cha nyuma niliwahi kupata muda kuchapisha historia za waandishi mbalimbali wachanga kwenye ukurasa wangu wa Facebook na Instagram kama sehemu ya kuwafanya wajulikane. Nilipata waandishi zaidi ya kumi, bado wapo kwenye kumbukumbu hadi leo kwenye ukurasa wangu. Jambo la pili ni kutangaza kazi zao wanapokuwa wanazindua ili kuwafanya wajulikane kwa kada ya wasomaji wangu. Tatu, nafikiri, kwa siku za mbele ni kufungua darasa la ulezi kwa walau nusu saa au saa moja kwa mwezi kuwafundisha waandishi wachanga bure. Sijajua bado nitalifanikisha vipi, lakini bado nafikiri namna bora ya kusaidia kwa njia hii.

Unaionaje Fasihi ya Kiswahili Sasa na kesho?

Fasihi ya Kiswahili inaendelea kukua—hivi sasa ni Lugha ya Kimataifa, japo si Lugha ya Umoja wa Mataifa. Ni jukumu la kila mwandishi kuhakikisha anaendelea kuandika ili kuchangia kukua kwa Kiswahili, lakini pia kuvuna matunda ya kukua kwa Kiswahili Barani Afrika, na hata nje ya Afrika.

RM

MJUE MTUNZI

Tukio la Kifasihi Lililowaweka Karibu Waandishi na Wasomaji

'Mkiwaunga mkono watakwenda na msipowaunga wanaweza kwenda' Mh. Adolf Mkenda (Mb)

TUKIO la Mjue Mtunzi ambalo huandaliwa na Umoja wa Waandishi wa Riwaya Wenye Dira (UWARIDI) limekuwa sherehe kubwa kati ya fanani na hadhira. Nachelea kusema kwamba hii haijawahi kutokea hapo kabla.

Lengo kubwa kabisa la tukio hili ni kuenzi, kuwatumuku na kuwatangaza waandishi na kazi zao za Kiswahili.

Umoja wa Waandishi wa Riwaya wenye Dira chini ya Rais wake Hussein Issa Tuwa ulikuja na ubunifu wa tukio hili la Mjue Mtunzi ambalo limekuwa kiunganishi kikubwa sana katika ya waandishi wa riwaya na wasomaji wao. Lilikuwa kama sherehe, *mtoko* wa wanafasihi Tanzania hususan katika Jiji la Dar es salaam. Mjue Mtunzi imekuwa nafasi ya waandishi kuwajua ana kwa ana wasomaji wao na wasomaji kuwajua ana kwa ana waandishi wao. Kupiga picha na kubadilishana mawazo; mambo yote haya yalivutia.

Kwakweli linabakia kuwa tamasha kubwa zaidi la vitabu nchini. Hakuna wa kupinga hili. Kitu cha kuvutia zaidi ni kile cha UWARIDI wenyewe kutoa Ngao za heshima kwa waandishi wake wa ndani na wacache kutoka nje yao.

Kama uliwahi kusikiliza vyombo vingi vya habari miaka ile ya tukio hili hautakuwa mbali na mawazo yangu kwamba Mjue Mtunzi ilikuwa inaenda kuisimamisha Afrika Mashariki na Kati katika suala zima la kuvitukuza vitabu na kuutukuza uandishi. Mengi yalifanyika kiubunifu zaidi; uzinduzi wa vitabu, ngao za heshima, mpangilio wa matukio na uwasilishaji wa kila kitu..

Tukifungua shajara yetu tunaona msimu wa kwanza wa tukio hili lililofayika tarehe 23 ya Mwezi wa Februari mwaka 2020 katika ukumbi wa Chuo cha Posta, Kijitonyama na kubebwa na kauli mbiu *Mjue Umsome, Msome Umjue*. Katika tukio hili kulikuwa na “Kiti cha Mtunzi” ambapo kati ya waliokikalia alikuwapo mwandishi Lilian Mbaga aliyezungumzia kitabu chake maarufu cha Hatinafsi na Hussein Tuwa aliyezungumzia safari yake ya kiuandishi hususan riwaya ya Mtuhumiwa. Mwandishi mwingine aliyeipamba siku hiyo alikuwa ni Lello Mmasi, mshindi wa Tuzo ya Mabati mwaka wa 2019.

Msimu wa pili wa tukio hili ulibamba kwelikweli pale Ilala katika ukumbi wa NSSF ambapo makumi ya vitabu vilizinduliwa kikiwamo Salome wa Sadaka cha David Shalali, Chawa cha Hussein Molito, Hiriki ya Tunu cha Joseph Shaluwa, Hawara cha Hafidh Kido na vinginevyo.



Mgeni rasmi Mheshimiwa Adolf Mkenda (MB) pamoja na wageni wengine mashuhuri katika Mjue Mtunzi msimu II



Waandishi waliozindua vitabu vyao wakiwa katika picha na Waziri wa Elimu mara tu baada ya uzinduzi huo.



Mwandishi Joseph Shaluwa akipokea Ngao ya Mtunzi kutoka kwa Waziriwa Elimu Mh. Adolf Mkenda

SHAJARA

sema ‘Thamini vya Nyumbani, Mjali Fanani’ liliileta serikali karibu kwa kumualika Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Adolf Mkenda (MB), naye katika hotuba yake alitoa wito kwa makampuni na taasisi mbalimbali kuunga mkono harakati hizi kwa kuanza na UWARIDI. Alisisitiza kuwa UWARIDI tayari upo na umejipanga.

Pamoja na mheshimiwa waziri kuzindua vitabu vya waandishi wa UWARIDI, katika tukio hilo pia zilitolewa ngao za heshima ambazo zilikuwa ishara ya kutambua mchango wa waandishi ndani ya UWARIDI na nje yake. Ngao hiyo ilikabidhiwa kwa Ibrahim Gama, Joseph Shalwa ambao ni waandishi wa UWARIDI na Elizabeth Mramba mwandishi kutoka nje ya umoja huo, ikiwa ni moja ya kuonesha kwamba UWARIDI ni kwa waandishi wote wa riwaya wanaoonesha dira ya maendeleo katika uandishi wao. Kwa kifupi waandishi wenye malengo chanya kwa kalamu zao.

Kama kumbumbu za Shajara yangu zipo sahihi nachelea kusema kwamba tukio hili la Mjue Mtunzi ndilo lili-lopelekea kuzaliwa kwa Tuzo Nyerere ya Uandishi Bunifu hapa Tanzania. Na kwa kudhihirisha umahiri katika uandishi wa riwaya, misimu yote mitatu ya kwanza ya tuzo hiyo waandishi kutoka UWARIDI wameng’ara.

Kongole kwao kwa kuwa pamoja na kukosa msaada kutoka wadau wa nje bado waliweza kuweka nguvuzao pamoja na kufanikisha tukio hilo. Hakika hii inaleta maana nzima ya herufi ya kwanza ya jina lao ‘U’ yaani Umoja.

Lakini wakati hadhira ikianza kupata ari ya kuongeza nguvu za usomaji wa vitabu ilizopigiwa chapuo na umoja huu ukimya uliotanda tangu msimu wa pili uliungwa mkono na Elite Bookstore unatutia shaka. Je tusubiri

msimu wa tatu au tugeuze nyuso zetu upande mwingine? Mko wapi UWARIDI? Waswahili wanasema ‘Kimya kingi kina mshindo mkuu’ nasi tunaubiri huo ‘Mshindo’ ambao tunaamini kuwa hautotikisa tu Tanzania bali Afrika Mashariki na kati yote.

RM



Pichani ni wanachama wa UWARIDI mbele ya duka l vitabu la Elite, Tangi Bovu, siku walipotembelea duka



Pichani ni washindi watatu wa Tuzo Nyerere ya Uandishi Bunifu msimu wa kwanza, wa pili na watatu. Kutoka kulia ni Hamis Kibari, Laura Pettie na Maundu Mwingizi. Wote ni wana-UWARIDI.

MEROME
COMPANY LIMITED
"Your Vision, Our Mission"

MEROME
COMPANY LIMITED
NI MABINGWA
wa kutengeneza

3D BANNER ZA 3D (MABANGO YA 3D)

BUSINESS CARD

T-SHIRT ZA WAFANYAKAZI

RECEIPT BOOKS

Karibuni sana wateja wetu

KWA MAWASILIANO ZAIDI:
+255 712 345 316

EMAIL:
meromecompany@gmail.com

Basi tukaendelea na visiwa kadhaa hata kukaelekea kwenye kisiwa cha mwisho ili tugeuze. Kwa jumla tulikuwa watu 48 wafanya biashara pamoja na manahodha na wasaidizi tulikuwa jumla ya watu 60.

Endelea...

Tulipokuwa tupo kwenye bahari tukielekea kisiwa kile ghafla nahodha alipoteza uelekeo na kutuambia amepotea na yupo kwenye kisiwa cha maharamia vibushuti. Hatukuelewa nini anazungumzia lakini alifafanua zaidi ni watu wafupi wanaotembea kwa makundi. Kazi yao ni kupora majahazi. Basi haukupita muda tukawaona wanakujia, nahodha aliongeza kuwa kupambana nao kwenye maji hatuwezi ila tukienda nchi kavu hawatakuja.

Nahodha alijitahidi awezavyo awahi kufika nchi kavu kwenye kisiwa kinachoonekana jirani. Hakuwahi kufanya hivyo tukavamiwa na jahazi letu likachanywa na kukatwa katwa na nanga ikakatwa. Walipora mali zetu zote na tukakimbilia kwenye kisiwa kile. Tukiwa tukihangaika nini tufanye kuondoka pale tukaona kuna jumba kubwa sana mbele yetu. Bila ya kujuwa kama ule ni mtego mwingine tukaingia kwenye jumba lile na kuanza kufanya mipango.

Usiku ulipofika tukaamua kujisitiri mule. Kumbe jumba lile ni mtego wa majidude yanayokula watu. Wanavizia wasafiri wanapopata matatizo na kuporwa wakiingia mule wanafungua na kuwala. Basi usiku ule likaja jitu moja kubwa sana na refu pia. Kwa urefu alonao nilimfikia magotini na upana wake lamda tujipange saba kama mimi. Ukiangalia ukubwa wa jumba lile utaamini ukubwa wa alolijenga.

Basi limtu lile lilipoingia likafunga mlango na kukoka moto. Tukiwa

tumetulia sana hatujui tufanye nini, lile limtu likaamza kumshikamshika kila mmoja. Likamkamata nahodha mkuu na kuanza kumbanika. Kumbe lilikuwa likiangalia mtu alionenepa amle. Alimbanika nahodha wetu na kuanza kumla. Alimla wote kisha akalala fofofoi. Kila mmoja alikuwa akitetemeka na kuanza kulia na kuogopa.

Lile limtu likalala pale mpaka ilipofika karibu na alfajiri likatoka na kuacha mlango wazi. Tulikaa pale ndani na baada ya muda tukatoka. Tulipofika nje tukaanza kupiga mipango ya kuondoka. Tulizunguka kisiwa kile kutafuta pa kulala lakini tulikosa. Tukiwa katika hali ilie nikapata wazo la kuwa tutengeneze mitumbwi midogomidogo. Tukaanza kufanya kazi ile hata usiku ukakaribia kuingia. Nikawashauri wenzangu kuwa tumuuwe yule mtu au tumtoboe jicho lake. Maana alikuwa najicho moja tu. Nikasisitiza kuwaambia kama tutamuwa ndo tutaweza kuondoka hapa bila hivyo atafuata na wenzie.

Tukapanga mpango wa kumuua na mimi nikiongoza mtego. Usiku ule tukaingia mule ndani na tukajifanya tumelala. Lile limtu likaingia na kuanza kumpapasa kila mmoja ili achukuwe alonona amle. Alimchukua nahodha mwengine alokuwa amenenepa zaidi katika sisi. Basi akambanika pale tukiwa tunamuona. Uchungu ulinishika lakini niliendelea kusubiri alale. Ali-polala tu nikaweka msumari wa moto kwenye mato na ukaiva vizuri hata ukawa mwekundu sana. Baada ya muda nikawdokoa wenzangu kuwa mambo tayari.

Nilimfata yule limtu na kumchoma n a msumari ule

kwenye jicho lake. Alilia sana na kuguta makelele. Alikwenda kukaa mlangoni ili atukamate. Kwakuwa alikuwa ni mrefu sana tuliweza kupita kwenye magoti yake hata bila kutupata. Tukaenda kwenye mitumbwi yetu na kuanza kuimalizia kwa msaada wa mbalamwezi. Lile limtu likaelekea sehemu huku linalia. Muda le kwa haraka zaidi tukamaliza mitumbwi yetu na tukagawana waiwi wawili kila mtumbwi.

Baada ya kugawana tukaanza kuingia maji kila mmoja anajitahidi kuenda kwa haraka kiasi awezavyo ili kuweza kuondoka kisiwa hiki. Basi baada ya jua kuchomoza tulikuwa mbali kidogo lakini tukashangaa tunaona weupe unakuja. Kumbe lile limtu lilikwenda kuwatafuta wenzie wengi wakiwa wamebeba mawe. Kwa urefu wao walianza kuyaingia maji na kuanza kuturushia mawe. Wenzetu walokuwa nyuma walizama kwa mawimbi ya maji baada ya kurushiwa majimawe makubwa. Mwishowe mitumbwi miwili tu iliokoka wakwetu na wawenzetu, hivyo tukawa wanne tulookoka.

Tulikwenda bila ya kujua wapi tutaishia, kwa bahati tukaona kisiwa kwa mbele zaidi. Tukaingia kwenye kisiwa kile na kuanza kutafuta chakula. Tukapata matunda na maji. Tuliandalanda pale na ilipofika jioni tulilala chini ya mti. Kwa ghafla usiku alikuja nyoka mbubwa sana na akamchukuwa mwenzetu aliyekuwa pembeni amelala. Tukaogopa sana maana tumeokoka kule kwenye mawatu na sasa ni nyoka. Kwa hakika usingizi haukuja tena.

Ilipofika asubuhi tulitafuta njia ya kurudi bila mafanikio basi nikawashauri wenzangu tutengeneze kitundu cha miiba tulale. . Itaendelea...

WAANDISHI bunifu wametakiwa kuzibidhaisha kazi zao kulifikia soko la kimataifa. Hayo yalisemwa katika warsha iliyofanyika kwenye tukio kubwa la **Mashariki Creative Economy Expo** lililoandaliwa kwa kushirikiana na Taasisi ya Utamaduni na Maendeleo Afrika Mashariki (CDEA).

Jukwaa hili liliwakutanisha wasanii, wabunifu, watajarishaji wa filamu, waandishi, wachapishaji na wadau wa sera kwa lengo moja kubwa: kuifanya sanaa, utamaduni na hakimiliki isiwe kitu cha kujifurahisha tu, bali iwe biashara inayoweza kumuingizia mbunifu kipato na kuchangia uchumi wa taifa.

Mashariki Expo 2026 ilifanyika Dar es salaam katika ukumbi wa Mlimani City kuanzia Agosti 18 hadi 21, ikiwa ni siku nne za matukio yaliyowakutanisha wadau mbalimbali wa ubunifu.

Katika moja ya matukio yaliyojiri katika siku hizo ni

meneja wa kampuni ya uchapishaji ya Mkuki na Nyota alieleza jinsi riwaya hiyo ilivyobadilika kutoka maandishi mpaka kuwa filamu. Bwana Tampiwa alikazia zaidi kuwa Kiswahili ni lugha inayoweza kubeba kazi zetu kiulimwengu. **RM**



MASHARIKI EXPO 2026 'Bidhaisheni Kazi Zenu Ili Kufikia Soko la Kimataifa'

lile la uzinduzi wa logo ya Copyright Friendly, ambapo mwanamuziki mkongwe kutoka Afrika Kusini Yvonne Chaka Chaka alitambulishwa kama Balozi. Mashariki Expo 2026 tungeweza kuiita 'shamba darasa' kwa maana ilikuwa sehemu ya wabunifu kujifunza na kutanua wigo wa ubunifu wao kwa kukutana na wabunifu wengine kutoka nje ya Tanzania.

Katika warsha ya *Literary Rights* iliyowahusu zaidi waandishi bunifu wa riwaya, mashairi, filamu na kadharika, mambo mengi yalizungumzwa, mawazo mengi yalichagizwa katika kutazama mustakabali wa uandishi katika ulimwengu huu wa akili unde. Mwakilishi kutoka PATA licha tu ya kutoa shukrani zake kwa kuwa mmoja wa washirika katika maandalizi ya tukio hilo pia alizungumzia tatizo la ushuru, usafirishaji na changamoto za usabazaji na ugumu wa vitabu vya Kiswahili kuingia kwenye majukwaa makubwa kama ya Kindle Publishing.

Katika meza ya mazungumzo (Paneling) iliyojumuisha wabunifu bobezi mbalimbali kutoka nchi tofauti iliyobebwa na mwongozo 'Biashara ya Haki za Kazi za Fasihi Barani Afrika: Mifano ya ukuzaji wigo, upatikanaji na uundaji wa thamani' ya kazi za uandishi bunifu. Katika mazungumzo hayo ilikaziwa sana kwa waandishi kubadili kazi zao kadiri ya ulimwengu unavyokwenda. Akitolea mfano riwaya ya Vuta N'kuvute, Tampiwa Muchechemera



Picha za matukiombalimbali yaliyojiri katika siku hizo.



SHUBAKA LA VITABU

Bado tunazidi kufungua shubaka la vitabu na kupata hazina kubwa ili-yojificha. Kama uliwahi kuisikia Misri ya kale na simulizi zake za kuisimua za mapiramidi na mafarao, basi katika safu hii Mervat Sakr anaendelea ku-kusimulia kuhusu 'Mapiramidi' ya fasihi kutoka Misri

Tawfiq al-Hakim

Inatoka toleo lililopita...

Jina la Tawfiq al-Hakim linahusishwa moja kwa moja na kile kinachojulikana kama "Tamthilia ya Wazo" (Masrah al-Fikra), mtindo wa tamthilia unaojengwa zaidi juu ya mijadala ya kifalsafa na maswali ya kiakili kuliko mfuatano wa matukio au migogoro ya kawaida ya kisanaa. Katika tamthilia zake, wahusika hubadilika na kuwa vyombo vya kutafakari mawazo, huku jukwaa likigeuka kuwa nafasi ya kujadili masuala ya uwepo wa mwanadamu, haki, mamlaka na maarifa.

Miongoni mwa tamthilia zake maarufu ni: "Ahl al-Kahf" (Watu wa Pangoni), inayochunguza uhusiano kati ya mwanadamu na wakati pamoja na changamoto ya kuendana na mabadiliko ya nyakati.

"Shahrazad", inayojadili mipaka ya maarifa, ukweli na fikra za kubuni.

"Al-Sultan al-Ha'ir" (Sultani Aliyechanganyikiwa), inayouliza maswali kuhusu uhusiano kati ya mamlaka, sheria na haki.

"Sulayman al-Hakim", inayochunguza hekima, mamlaka na majaribu ya mwanadamu.

"Al-Aydi al-Na'ima" (Mikono Laini), inayozungumzia mabadiliko ya kijamii pamoja na mgongano kati ya fikra na vitendo.

Katika kazi hizi zote, Tawfiq al-Hakim hakutoa majibu ya moja kwa moja, bali alimshawishi msomaji au mtazamaji kufikiri na kutafakari, huku akiacha maswali wazi bila kuyafunga kwa hitimisho moja.

Riwaya na Fikra za Kijamii: Ubunifu wa Tawfiq al-Hakim haukuishia katika tamthilia pekee, bali ulihusisha pia riwaya na maandiko ya kifikra yaliyogeuka kuwa miongoni mwa kazi za msingi katika fasihi ya Kiarabu. Katika riwaya yake *"Yawmiyyat Na'ib fi al-Aryaf"* (Shajara ya Nambu wa Mashtaka Vijijini) aliwasilisha taswira halisi ya mfumo wa mahakama katika maeneo ya vijijini na kufichua matatizo ya urasimu na ufisadi.

Katika *"Usfur min al-Sharq"* (Ndege Kutoka Mashariki) alilinganisha ustaarabu wa Mashariki na Magharibi kupitia safari ya mhusika aliyeishi kati ya tamaduni hizo mbili. Aidha, *"Awdat al-Ruh"* (Kurudi kwa Roho) iliakisi ari ya utaifa wa Misri na mchango wake katika kuamsha jamii, huku "Himar al-Hakim" (Punda wa Al-Hakim) ikiwa kazi iliyochanganya kejeli na falsafa kwa ustadi mkubwa, na kuonyesha uwezo wake wa kugeuza matukio ya kawaida ya kila siku kuwa tafakuri za kina kuhusu maisha.

Mtindo wa Uandishi: Mtindo wa Tawfiq al-Hakim ulijulikana kwa kuunganisha lugha rahisi na mawazo yenye kina. Hakulenga mapambo ya lugha, bali alijitahidi kuwasilisha wazo kwa uwazi na ushawishi mkubwa. Maandishi yake yalitofautishwa na sifa kadhaa, zikiwemo:

• Kutegemea ma-zungumzo kama njia ya kufichua mawazo.

• Matumizi ya ishara na taswira badala ya maelezo ya moja kwa moja.

• Kuweka mkazo katika migongano ya fikra kuliko migongano ya kimatukio.

• Kuunganisha fasihi na falsafa katika mfumo mmoja wa kisanaa.

• Kumwachia msomaji nafasi ya kutafsiri na kutafakari maana mbalimbali za maandishi.

Kwa sababu hiyo, kazi zake zimeendelea kusomwa na vizazi mbalimbali, kwani maswali aliyoyaibua haya-fungwi na wakati fulani bali hubaki na umuhimu katika kila zama.

Heshima na Utambuzi wa Kimataifa: Tawfiq al-Hakim alipata heshima kubwa ndani na nje ya Misri. Kazi zake zilitafsiriwa katika lugha nyingi, zikiwemo Kiingereza, Kifaransa na Kirusi, na tamthilia zake zika-onyeshwa katika majukwaa mbalimbali ya kimataifa, jambo lililochangia kuitambulisha fasihi ya Kiarabu kwa hadhira pana duniani. Aidha, alitunukiwa tuzo na nishani nyingi, zikiwemo Nishani ya Mkufu wa Jamhuri mwaka 1958, Tuzo ya Taifa ya Kutambua Mchango katika Fasihi mwaka 1960, na mwaka 1954 akachaguliwa kuwa mwanachama wa Baraza la Lugha ya Kiarabu, kama ishara ya kuthamini mchango wake mkubwa katika fasihi na fikra za Kiarabu.

Urithi Usioffia: Mpaka alipofariki dunia mnamo mwaka 1987, Tawfiq al-Hakim aliendelea kuwa mmoja wa waandishi wenye ushawishi mkubwa zaidi katika fasihi na fikra za Kiarabu. Aliibadilisha tamthilia kutoka kuwa chombo cha burudani na kuifanya kuwa jukwaa la tafakuri ya kifalsafa, huku akiigeuza fasihi kuwa njia ya kumwelewa mwanadamu na kuhoji mitazamo yake.

Hadi leo, kazi zake bado zinasomwa, zinafundishwa na kutafsiriwa, kwa sababu hazitoi majibu ya mwisho bali hufungua milango ya fikra na kumwalika msomaji kutafuta majibu yake mwenyewe. Kwa sababu hiyo, Tawfiq al-Hakim ameendelea kubaki katika historia ya utamaduni wa Kiarabu kama mwandishi aliyeifanya tamthilia kuwa "Tamthilia ya Wazo", na fasihi kuwa safari ya kudumu ya kutafakari kina cha maisha ya mwanadamu.

Imetayarishwa na Mervat Sakr — Cairo, Misri

KITABU NILICHOSOMA

NEXT GENERATION LEADER

Mwandishi: Andy Stanley
Kitabu: Next Generation Leader
Msomaji: Erick Mbise.

Mambo yanayomtengeneza kiongozi mzuri.

1. Uwezo (Comptence)

Ukitaka kuwa kiongozi mzuri ni vyema ukawa na uwezo mzuri katika eneo unaloongoza. Mwandishi Andy Stanley anasema viongozi wengi wachanga wanakosea maana wanafanya sana kuliko kuongoza wengine kufanya. Anasema wengi wanafanya wakijua ndio njia itakayowafanya waonekane wachapa kazi. Kiongozi unatakiwa uwape watu nafasi ya kufanya majukumu na wewe utimize majukumu yako. Usiwe meneja unayetaka kufanya kila kitu mwenyewe. Kiongozi angalia eneo lako ambalo unaweza kufanya vizuri na usimame nalo.

Unaweza usiwe kiongozi ila katika taasisi unayofanya kazi angalia ni eneo gani unaweza kufanya vizuri. Hii itakupa ubora kuliko kufanya kila eneo na mambo mengine hayaipo katika ubora maana sio eneo lako. Hii haikunyimi kujifunza mambo mapya ila inakupa urahisi maana taasisi ina watu wengi. Unaweza pia kuangalia katika taasisi unayofanya kazi ni maeneo gani yana mapungufu kisha ukatafuta ujuzi katika hayo maeneo na kuja kufanya kwa ubora na kuwa mtu wa kipekee katika taasisi.

Kama kiongozi zingatia haya mambo.

*** Mamlaka na ujuzi**

Haimaanishi kwasababu una mamlaka katika taasisi uingilie kila eneo. Kama hauna ujuzi na eneo fulani waache wenye ujuzi wafanye kazi, unapoingilia majukumu ya watu kazini kwa kutumia mamlaka utaharibu ubora wa miradi katika taasisi.

*** Hauwezi kuwa na uwezo katika kila eneo.**

Kama kiongozi tambua unaweza

kuwa na udhaifu. Hauwezi kufaa katika kila taasisi au kila idara hivyo ni vyema kujua eneo unaloweza kufanya kwa ubora. Mtu anaweza kufanya vizuri katika kutafuta wateja lakini katika kufanya mauzo na kufuatilia asiwe mzuri.

*** Kuwa tayari kutengeneza viongozi wengine.**

Kwa viongozi vijana ni changamoto kutengeneza viongozi wakihisi nafasi zao zitachukuliwa. Lakini pia viongozi wengine wanaamini wakifuatilia jambo wenyewe ndio litakua katika ubora. Kumbuka uongozi haulengi kufanya mambo katika ubora pekee ila kutengeneza wengine uwezo wa kufanya vitu katika taasisi.

2. UJASIRI

Kiongozi lazima awe na uthubutu, awe tayari kufanya vitu ambavyo huenda watangulizi wake hawakua tayari kuvifanya. Ili taasisi iwe hai inahitaji kuwa na mabadiliko na katika kuleta mabadiliko ni lazima awepo kiongozi ambaye yupo tayari kufanya mabadiliko.

Hofu ya kuchukua hatua mpya ni mbaya kwa kiongozi na kama ungewauliza viongozi wengi wazee watakuambia katika kitu wanajutia ni kuogopa kuchukua hatua.

Maeneo matatu yanayoonyesha ujasiri wa kiongozi.

*** Ujasiri wa kusema hapana**

Haya ni maamuzi magumu, kusema hapana kwa jambo ambalo halitainufaisha taasisi yako. Siyo kila mlango unaogongwa ni fursa, wakati mwingine unapaswa kusimama na jambo moja na kushughulika nalo. Hata kama zitakuja fursa nyingine nyingi lakini angalia kwanza uelekeo wako sahihi kutimiza jambo moja.

*** Kukubali uhalisia.**

K a m a

vyema

uhalisia wa mambo. Kuna wakati yanahitajika mabadiliko lakini kama mabadiliko hayatafanyika kwa kuukubali ukweli taasisi itazama. Kwanini unaandaa sherehe wakati ulipata hasara?

***Ujasiri wa kuwa na ndoto kubwa.**

Mafanikio makubwa yalianzia katika ndoto kubwa. Hauwezi kufanya mambo makubwa kama una ndoto ndogo, ruhusu akili yako iwaze mambo makubwa ambayo watu wengine wanaweza kuona ni mambo yasiyowezekana.

3. KUWA NA KOCHA

Kuwa kiongozi mzuri unahitaji kocha ambaye atakua anakufanyia tathmini. Ni kweli unaweza kujipima mwenyewe lakini ukipata mtu wa pembeni anaweza kukupa majibu mazuri zaidi juu ya kile unachopima.

Kocha anafanya mambo matatu muhimu

- a) kukuangalia
- b) Kukuelekeza
- c) Kukutia moyo.

4. KIONGOZI MZURI ANA TABIA NJEMA NA MUADILIFU.

Kama tulivyojadili hapo awali, unaweza kuongoza bila tabia. Lakini tabia ndiyo inayokufanya kuwa kiongozi anayestahili kufuatwa. Unaweza kutumia uongozi kuongoza watu lakini mwisho wa siku tabia yako itabakia na jina lako. Hata ukistaafu tabia zako ndizo zitabakia kukumbukwa. Tabia ni kufanya yale unayopaswa kufanya hata kama unaona ni magumu. Tabia inahusianisha usahihi wa kufanya mambo yanayopaswa kufanya, tabia ni namna ya maisha ya kila siku.

Imechambuliwa na Eric Mbise
Anna Mbise Pan-African Mobile

HABARI PICHA

Matukio ya wanafasihi



WASHRIKI katika Mashariki Expo 2026 katika picha ya pamoja



Mwandishi Richard Mwambe akiwa katika mazungumzo na Dkt. Utah Reusta Jahn



Hussein Wamaywa akibadilishana mawazo na Mzee Madaraka Nyerere katika Mashariki Expo 2026.



PICHA YA MFANO: Mwandishi wa FATINA, Gwamaka Mwamasage pamoja na bintiyake (katikati) na mzazi mwenziwe, katika mahafali ya binti huyo.

Ngurumo ya Mwandishi tunampongeza mwandishi huyu kwakuthamini uzao wake. Pichakwa hisani ya Gwamaka



Pichani ni Mkurugenzi na mwasisi wa TUNGO TATA TV Bakari Mwinshehe (mwenye balaghashia) akiwa na Mkurugenzi na mwanzilishi wa Jarida la Ngurumo ya Mwandishi Bw. Richard

MALENGA WA KILEO

FURAHA

Furaha toka moyoni
Yatuweka furahani
Yaificha kimyani
Inayotessa huzuni

Furaha ilo usoni
Ndo itokayo moyoni
Yatutakasa mwilini
Na Kutenda kwa makini

Furaha ni kituchema
Kinachotfanya twahema
Kwetu hakuna mahema
Wala asiye rehema

Si kinababa si kinamama
Kwetu kede ni wema
Furaha tunayoisema
Ndo hiyo tunanema

Bubujiko la furaha
Latweka mbali na karaha
Daima siye tuna raha
Kabila yetu furaha

Cheka bwana acha unaa
Kipi chakupa kinyaa
We cheka kila saa
Hakuna wa kukuona kichaa

Kucheka ndiyo dawa
Tangu Adamu na Hawa
We mbona wachachawa
Waogopa lako bawa

Cheka bwana, nononono unamnunia nani?

Shujaa Maneno!

TAHARIRI

Salamu nyingi sana kwenu nyote!

Hakika kwa kujipatia Jarida la Ngurumo ya Mwandishi basi utaona usikoona.

Sisi tunayo furaha sana kuwa nawe tena katika toleo hili la 54, na nikujulishe tu kuwa sasa tumetimiza miaka mitano ya kukuletea burudani hii ya kipekee Tanzania na Afrika.

Haya ni matokeo ya kuona tusikoona lakini *paap!* Tumefika. Kwakweli tunajivunia hili na tunakushukuru sana kwa mchango wako. Jarida hili limewavutia wanazuoni wengi na limeshaanza kuongelewa kimataifa, je nini kinafuata?

Sisi yetu macho na matumaini kuwa ipo siku Ngurumo ya Mwandishi litanguruma pande zote nne za dunia. Lakini yote kwa yote, ninyi wasomaji ndiyo kila kitu, mnalipeleka jarida pahala ambapo sikuwahi kufikiri, mnalifikisha kwa watu ambao sikuwahi kufikiri. Asanteni sana kwa hili na muendelea na moyo huohuo.

Jarida hili kama sehemu ya burudani lakini pia lina toa elimu kubwa sana kwa jamii inayolisoma. Shuhuda nyingi zinatufikia mezani na hata wengine wana diriki kusema jarida hili lichapwe nakala ngumu. Ndiyo! Nasi tunapokea ushauri wote huo na tunatumaini kuwa ipo siku yaweza kuwa.

Katika toleo hili la 54 ambalo limebeba kaulimbiu 'ONA USIKOONA' linakujia na makala maalum inayodadavua miundo ya Lugha ya Kiswahili. Huu ni moja ya mchango kutoka kwa mlumbi wa Kiswahili katika ukanda wa Afrika Mashariki ambaye ameona umuhimu wa kukusaidia wewe mwandishi na we msomaji kujua 'uundaji' wa silabi katika lugha yetu adhimu ya Kiswahili. Ngurumo ya Mwandishi si tu kwa burudani bali limesheheni elimu kwako kama mzazi, mwandishi, mwanafunzi nk. Hivyo ukilipata jarida hili lisambaze kwa wengine.

Kwa kulisoma, hakika utaona usikoona.

Basi usiache kuzingatia ukurasa wa 35, ili tule Kris-mass pamoja.

Wakatabahu!

Amata Ric Richard Mwambe

KITABU MARKET—Bookshop

new text



OPERESHENI KASHMIR

Sasa Kinapatikana
kwa Tsh

15,000/=

JIKAMATIE
NAKALA YAKO

DAR ES SALAAM
Duka la Kona ya
Riwaya
Kinondoni Morocco

Simu:
0655428085

Zammira

new text



OPERESHENI KASHMIR

Sasa Kinapatikana
kwa Tsh

15,000/=

JIKAMATIE
NAKALA YAKO

ARUSHA
Nje ya Duka
KIMAHAMA

Simu
+255 757 690 302

ALLY SAID

www.kitabumarket.co.tz

KINAPATIKANA ARUSHA

Kinapatikana Kwa Ally Said Shaban, nje
tu ya KIMAHAMA Bookshop

Simu: 0757690302 na 0656744390



15,000/=
tu

Jipatie Nakala
Yako Sasa! 🌟

MSALITI

15,000/=

Kona ya Riwaya
BOOKSHOP

Fika dukani kwetu au
wasiliana nasi Kwa
Simu

0655 428 085

**Mliopo mikoani
tunakutumieni.**

KUTOKA MAKTABA WILLIAM SHAKESPEAR

WILLIAM SHAKESPEARE (1564–1616) ni mwandishi wa michezo ya kuigiza na mashairi kutoka Uingereza, ambaye anachukuliwa kuwa mmoja wa waandishi wakubwa na wenye ushawishi mkubwa zaidi katika historia ya fasihi duniani.

Vijana wa kizazi cha sasa wengi hawajawahikumsikia mtu huyu mashuhuri katika uga huu wa fasihi. Kupitia Ngurumo ya Mwandishi, mjue jagina huyu.

William Shakespear alizaliwa mwaka 1564 huko Stratford-upon-Avon, Uingereza, Mwishoni mwa miaka ya 1580 au mapema miaka ya 1590, Shakespear alihamia London ambako alifanya kazi kama mwigizaji, mwandishi, na mmiliki mwenza wa kundi la waigizaji lililojulikana kama Lord Chamberlain's Men (*baadaye The King's Men*). Pia walikuwa wamiliki wa uwanja maarufu wa michezo wa The Globe Theatre. Mwanafasihi huyu nguli alifariki tarehe 23 Aprili 1616 akiwa na umri wa miaka 52.

Katika maisha yake Shakespeare aliacha urithi mkubwa wa maandiko uliogawanyika katika makundi makuu matatu:

Kundi la kwanza lilihusisha uandishi wa michezo ya Simanzi/Huzuni (*Tragedies*). Katika uandishi huu wa Simanzi, Shakespear ametuachia kazi zifuatazo

1. **Hamlet** – Inayozungumzia kisasi, wasiwasi wa nafsi, na usaliti.
2. **Romeo and Juliet** – Hadithi maarufu duniani ya wapendanao waliokutana na mkasa wa kifo.
3. **Macbeth** – Inayoonyesha athari za tamaa mbaya ya madaraka.
4. **Othello** – Inayoelezea wivu na usaliti (*mchezo ambao Baba wa Taifa Mwl. Julius Nyerere alitafsiri kwa Kiswahili*).
5. **King Lear** – Inayohusu uzee, madaraka, na usaliti wa kifamilia.

Kundi la pili lilihusisha michezo ya kuchekesha / Futuhi (*Comedies*). Katika uandishi huu wa futuhi Shakespear ametuachia michezo kama

1. **A Midsummer Night's Dream**
2. **The Merchant of Venice** (*pia ilitafsiriwa na*

Baba wa Taifa Mwl. Julius Nyerere kama Mabepari wa Venisi)

3. Twelfth Night

4. Much Ado About Nothing

Kundi la tatu ni michezo ya kihistoria, (*Histories*) hii ni michezo inayoelezea maisha ya wafalme wa Uingereza kama vile Henry V, Richard III, na Julius Caesar.

Lakini pia Shakespear aliandika Mashairi (*Sonnets*) 154 (mashairi yenye mistari 14 kila moja) yanayozungumzia mada za mapenzi, uzuri, muda, na kifo.

Mchango Wake Katika Lugha na Fasihi:
Ushawishi wa Lugha: Shakespeare alileta mabadiliko makubwa katika lugha ya Kiingereza kwa kubuni na kutumia maelfu ya maneno na misemo mipya ambayo inatumika mpaka leo (k.m., "break the ice", "love is blind", "all that glitters is not gold").

Pamoja na kwamba aliishi miakamingi nyuma, kazi zake bado zinasomwa na kuigizwa ulimwenguni kote kwa sababu zinazungumzia tabia za mwana-damu ambazo hazibadiliki na wakati: mapenzi, chuki, tamaa ya madaraka, wivu, na hofu.

Katika toleo lijalo, tutaichambua hadithi ya Romeo and Juliet ili kunja kilichoma ndani yake.

Imeandalwa kwa msaada wa mtandao



William Shakespear

1564–1616

ELIMU JAMII

SAFARI YA MALEZI—12

10.0 FAMILIA KAMA SHULE YA KWANZA YA MALEZI

Familia ndiyo taasisi ya kwanza kabisa ambayo mtoto huikuta anapoingia duniani. Kabla hajafika shuleni, kanisani, msikitini au katika jamii pana, mtoto huanza kujifunza maisha ndani ya familia. Hivyo, familia inaweza kuitwa shule ya kwanza ya malezi kwa sababu ndani yake mtoto hujifunza lugha, maadili, tabia, mahusiano, wajibu na namna ya kuishi na watu wengine.

Malezi ya mtoto hayaanzi anapoanza shule, bali huanza tangu anapozaliwa. Kila tendo, neno au mfano anaouona kutoka kwa wazazi na walezi wake humjengea msingi wa maisha yake ya baadaye. Mtoto anayekulia katika mazingira yenye upendo, heshima na uwajibikaji huwa na uwezekano mkubwa wa kukua akiwa mtu mwenye maadili mema na mchango chanya katika jamii.

Katika dunia ya leo, familia nyingi zinakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile mabadiliko ya teknolojia, shughuli nyingi za kiuchumi, migogoro ya kifamilia na kupungua kwa muda wa wazazi kuwa pamoja na watoto wao. Hali hii imeathiri kwa kiasi fulani jukumu la familia kama shule ya kwanza ya malezi. Hata hivyo, licha ya changamoto hizo, familia bado ndiyo msingi mkuu wa malezi bora.

10.1 Maana ya Familia

Tuanguale kwanza maana ya familia, ili tuweze kufahamu umuhimu wake na faida zake. Familia ni kundi la watu wanaounganishwa kwa uhusiano wa damu, ndoa au malezi, wanaoishi pamoja au kushirikiana maisha kwa karibu. Familia ndiyo kitovu cha ukuaji wa mtoto kimwili, kiakili, kihisia na kijamii. Na kama tunavyofahamu umuhimu wa kitovu kwa mtoto kuanzia tumboni kwa mama yake hali kadhalika anapozaliwa, familia ndiyo inayobaki kuwa kitovu chake kikuu, kwa malezi, mahitaji yake nk.

Ndani ya familia, mtoto hupata mahitaji yake ya msingi kama chakula, mavazi, makazi, usalama na upendo. Lakini zaidi ya hayo, hupata nafasi ya kujifunza maadili na tabia zitakazomsaidia katika maisha yake yote.

Kwa Nini Familia ni Shule ya Kwanza ya Malezi?
Mtoto hujifunza lugha kwanza nyumbani:

Lugha ya kwanza mtoto hujifunza kutoka kwa wazazi na watu wa karibu naye. Kupitia mazungumzo ya kila siku, mtoto hujifunza namna ya kuwasiliana, kuuliza maswali na kueleza hisia zake. Vile anavyojifunza ndivyo atakavyovionyesha katika jamii na katika makuzi yake, hivyo kama wazazi na walezi wanapaswa kuwa makini sana katika kumlea mtoto katika hatua hii ya awali.

Mtoto hujifunza maadili ya msingi: Maadili kama ukweli, uaminifu, heshima, ushirikiano na uvumilivu huanza kufundishwa nyumbani. Watoto wengi huiga kile wanachokiona kuliko kile wanachoambiwa. Hivyo wazazi wanapaswa kuwa mfano bora wa maadili wanayotaka kuwaona watoto wao wakiyafuata.

Familia humjengea mtoto hisia za usalama: Mtoto anayehisi kupendwa na kuthaminiwa huwa na uwezo mkubwa wa kujiamini na kukabiliana na changamoto za maisha. Familia yenye upendo humsaidia mtoto kukua akiwa na afya njema ya akili na hisia. Watoto wengi waliopitia katika familia ambazo walikuwa wananyanyaswa huwa wanakosa kujiamini pindi wanapokuwa wakubwa, hivyo familia zinapaswa kuwa makini na aina ya malezi wanayoyatoa.

Familia Humfundisha Uwajibikaji: Kupitia kazi ndogo ndogo za nyumbani, mtoto hujifunza kuwajibika. Anaelewa kuwa kila mwanajamii ana jukumu lake na kwamba mafanikio yanahitaji juhudi na nidhamu. Hivyo kuna umuhimu wa kumfundisha mtoto kufanya kazi hasa zile ndogondogo ambazo zinaendana na umri wake.

10.3 Wajibu wa Wazazi Katika Malezi

Wazazi ni walimu wa kwanza wa watoto wao. Wana jukumu la kuhakikisha kuwa watoto wanapata mazingira mazuri ya kujifunza na kukua. Wajibu huu unahusisha:

- Kutoa upendo na matunzo, kusikiliza watoto na kuelewa mahitaji yao, kufundisha maadili mema, kutoa mwongozo na ushauri, kuweka nidhamu kwa njia inayojenga na kuwa mfano mzuri katika maneno na matendo.

Na. KELVIN JOHN
KYARA

0753767930

ELIMU JAMII

Malezi bora hayategemei utajiri wa familia bali yanategemea namna wazazi wanavyoshiriki katika maisha ya watoto wao. Wazazi wanaotenga muda wa kuzungumza na watoto wao hujenga uhusiano imara unaorahisisha malezi.

10.4 Changamoto Zinazoikabili Familia Katika Malezi

Katika karne ya sasa, familia nyingi zinakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazoweza kudhoofisha malezi. Miongoni mwa changamoto hizo ni:

- Matumizi makubwa ya simu na mitandao ya kijamii, ukosefu wa muda wa wazazi kutokana na shughuli za kiuchumi, migogoro ya kifamilia, ushawishi mbaya kutoka kwa marafiki na mazingira na kupungua kwa mawasiliano ndani ya familia.

Changamoto hizi zinahitaji wazazi kuwa makini zaidi ili kuhakikisha kuwa watoto wanapata malezi yanayowajenga kuwa watu bora. Wazazi wanapaswa kuwa makini sana katika malezi hasa kutoa muda wa kuwasiliana na watoto wao kujua changamoto wanazopitia, kufahamu marafiki wa mtoto kama ni wazuri au wabaya pamoja na kuwaongoza katika machaguo mema ya maisha yao ya baadae.

10.5 Hitimisho

Familia ni shule ya kwanza na muhimu zaidi katika maisha ya mtoto. Msingi unaowekwa nyumbani huathiri maisha ya mtoto kwa kiwango kikubwa, hata anapokuwa mtu mzima. Wazazi na walezi wanapaswa kutambua thamani ya jukumu lao na kuhakikisha kuwa wanatoa malezi bora yanayojenga maadili, uwajibikaji, heshima na upendo. Jamii bora huanza na familia bora, na familia bora huanza na malezi bora

Familia wakicheza pamoja. Hii nayo ni namba ya malezi ya kufundisha watoto upendo kati yao.



KWAHERI KINYANGULI TUZO 'KING KINYA'



**MCHORA KATUNI
KING KINYA AFARIKI DUNIA**

MCHORA katuni maarufu Tanzania Kinyanguli Tuzo au King Kinya amefariki dunia tarehe 17 ya Septemba 2026 baada ya kuugua kwa kipindi kifupi.

King Kinya aliyehudumu kwenye magazeti ya mwananchi na The Citizen kwa miaka 17 kama mchora katuni alianza kuugua akiwa nyumbani kwake Tabata mwanzoni mwa Julai mwaka huu hali iliyomfanya kukaa ndani kwa muda kabla ya kupelekwa kwao Morogoro.

Kaka wa marehemu alipokuwa akizungumza na gazeti la Mwananchi alisema Kinya akiwa Morogoro hali yake ilizidi kuwa mbaya na baadae alipelekwa hospitalini na kupewa rufaa ya kwenda Hospitali ya Mloganzila alikolazwa kwa juma moja kabla ya kuruhusiwakureje nyumbani.

Baada ya hapo, Kinya aliendelea kuumwa na kuanza kutapika na kuharisha, alirudi nhospitali na kupatiwa dawa kisha kurejea tena nyumbani na baadae alifariki.

King Kinya amezikwa katika makaburi ya Mwananyamala, Dar es salaam.

Hakika sote tu wa Mola na kwa Mola tutarejea.

Kwaheri King Kinya, kwaheri ya kuonana!

K.O.K.W.A—3

Ilipoishia...

“Ndiyo, mbona unaniuliza?” Amata akajibu na kumtwanga swali.

“Aaaa... hapana! Utalipia Ariary 25,000 tu,” yule dereva akamwambia Amata. Hata hivyo Amata alijua kuwa lipo jambo, kwanini dereva yule amwangelie kwa mshtuko namna ile?

Endelea...

“Sina Ariary kwa sasa... nina dola tu!” akamjibu yule dereva.

“Sawa! Dola tano tu za Kimarekani,” akatamka huku akiwasha gari na kuondoka zake.

Cocodu Hotel ilisheheni watu usiku huo. Amata aliteremka kwenye lile taksi na kuvuta hatua taratibu kuelekea kaunta iliyokuwa ikionekana eneo hilo. Alijitahidi kupenya katikati ya watu mpaka alipoifikia kaunta ile. Katika viti virefu vilivyopangwa kwa ustadi mbele ya hilo dirisha la mauzo waliketi watu tofauti tofauti, kila mmoja alionekana kuwa na hamsini zake. Wachache walikuwa wakiongea na kufurahi kwa uwazi. Upane mwingine palikuwa na watu walioonekana kuzungumza mazungumzo nyeti. Waliinamiana na kunong’ona. Warembo nao hawakuwa mbali na mavazi yao ya kuvutia usiku huo. Upane wa pili palikuwa na jengo la ghorofa sita na kibao kikubwa kilichosomeka ‘Concodu Hotel’.

“Nikusaidie!” sauti ya mhudumu ikamfikia Amata hata kabla hajajiweka vyema.

“Oh! Asante sana mrembo, upande wa swimming pool kuna nafasi nzuri ya kuketi?” akamuuliza.

“Ndiyo zipo, lakini kuna vurugu sana kwa sasa watu wanaoagelea ndiyo maana tumehamisha wateja wetu...” yule mhudumu akamjibu Amata. Amata akaitazama saa yake tena. Muda ulikuwa ukiyoyoma kwelikweli. Zilibaki dakika chache tu ili miadi aliyofuata itimie.

“Nitaketi huko... nipatie Mojito tafadhali!” akamwambia yule mhudumu.

“Na barafu au bila?”

“Na barafu please...” Amata akajibu huku akiongoza njia kama alivyoelekezwa kuelekea upande wa bwawa la kuogelea.

Amata aliwasili eneo husika, eneo la miadi na kulakiwa na watu wengi waliokuwa waniburudika kwa maji safi, baridi ndani ya bwawa lile. Wanawake warembo



na vijana mashababi walikuwamo. Ndani ya bwawa lile kila burudani iliendelea. Ukiachana na muziki wa DJ, waogeleaji walikuwa na burudani zao. Kamanda Amata aliangaza macho yake huku na huko kutazama kama kuna yeyote ambaye atamhisi ndiye mhusika wa miadi ile. Kwenye viti vilivyowekwa eneo hilo palikuwa na watu wachache sana ukiachana na wale waliokuwa kwenye maji. Katika wote hao, hakumuona ambaye hisia zake zilinaswa naye. Akatafuta kiti kizuri na kuketi. Haikupita dakika mbili akaletewa kinywaji alichogiza. Akajipapasa kiunoni pake, bastola yake ilikuwa makini. Akapeleka mkono kwenye mkoba wake na kutoa kizuia sauti cha bastola hiyo. Akakifunga. Kishapo akaiweka vizuri ndani ya koti lake. Punde tu, katika eneo lile aliingia mwanaume mmoja mwenye tambo kubwa. Ungemwona, kwa harakaharaka

ungesema ni mwarabu. Lakini hapana. Huyu alikuwa mmadagaska, mweupe kabisa. Mkononi mwake alikuwa na briefcase nyeusi huku yeye mwenyewe kavalia suti nyeupe. Mwendo wake tu ulikuwa wa kujiamini, kwani hakuwa anaonesha kuogopa lolote.

Akatembea mpaka kwenye moja ya meza ambayo alioneshwa na wahudumu. Akaketi. Palionekana kuwa na mazungumzo kidogo kisha wale wahudumu wakaondoka. Akabaki peke yake. Huyu aliyavuta macho ya Amata. Muda wote huo alikuwa akimtazama kwa makini na kuangalia mazingira kama kuna mikia nyuma yake au vipi. Yule bwana kila wakati alikuwa akiangalia saa. Ndiyo! Saa ya miadi ilikuwa imeshafika. Moyo wa Amata ulikuwa ukienda mbio. Hakujua na hakuwa na uhakika kama mtu huyo kaja peke yake au la. Nitafanya ninachoweza, labda kwake nitapata kitu kingine! Akawaza.

Muda ulikuwa umemwacha sana Amata. Katika kazi aliyotumwa na bosi wake, Madam S, hakutakiwa kufika huku kote. Ilikuwa tu palepale Louvre Hotel, ni kuipata ‘kokwa’ ambayo tajiri la Kirusia Mikhail Planchkov alikuwa nayo. ‘Ukimpata Planchkov...utajua kila kitu kuhusu kokwa, tunahitaji irudi Tanzania. Wewe unajua umuhimu na kazi yake...’ sauti ya bosi wake ilirindima masikioni, mpaka ikaufanya mwiliwe usisimke. Tayari mpaka hapo, Amata alishacheza patapotea. Ndege aliyopaswa kuondoka nayo ilikuwa bado dakika chache iache ardhi ya kisiwa hicho kikubwa Afrika.

Miezi Mitatu Nyuma

Dar es salaam

Katika jumba la Makumbusho jijini Dar es salaam hali ilikuwa tete. Ni siku hiyohiyo ambayo uzinduzi wa mfumo tepe uliojulikana kama ‘kokwa’ ulifanyika katika ukumbi maalum ndani ya jengo hilo na baada ya saa saba tu Kokwa ile ilitoweka katika mazingira ya kutatanisha. Wakuu wa usalama walikuwa hapo wakijadiliana hili na lile. Utata!

“Imewezekanaje kwa mtu kufika pale na kuchukua Kokwa?” Inspekta Simbeye akawauliza aliokuwa nao. Lakini kila mmoja hakuwa akijua kilichotokea. “Kwa jinsi ulinzi ulivyo na wataalamu wetu walivyosuka, mtu wa kawaida hawezi kabisa kusogea eneo hilo... hapa ni mawili; ama mmoja wataalamu wetu katoa siri ya kiusalama au tumezungukana wenyewe... wekeni hilo kichwani,” Simbeye akamaliza kusema. Akavuta hatua na kuingia eneo ambalo Kokwa ile iliwekwa kama sehemu ya maonesho. Utepe wa njano ulikuwa umezunguka. Ni chumba kikubwa kilichotandikwa zuria jekundu na kuficha sakafu yote. Ukiacha sehemu za kuzunguka watu wanaohitaji kuona kitu hicho, paliwekwa utepe mwekun-

du ulioshikizwa kwenye nguzo nane kwa umbo mraba. Katika yake kulikuwa nguzo ndogo ya urefu wa mita moja na juu yake palikuwa na kitu kama sahani ya kioo ambayo kwayo Kokwa ile iliwekwa. Na juu kabisa kulikuwa na taa maalum iliyokuwa ikimulika kwenye hiyo kokwa tu.

Usalama wa eneo hili ulikuwa mkubwa sana. Huwezi kuingia eneo ambalo kokwa ile iliwekwa pasi na kutambuliwa na vifaa maalum vya kielektroniki. Vifaa hivyo vitahitaji kutambua alama zako za kiganja mkono wa kuume, jicho la kushoto pamoja na sauti yako ukitamka neno maalum ‘Kokwa’. Na ni watu wawili tu waliokuwa na uwezo wa kufika eneo hilo, nan i lazima wawe wote wawili kwa kuwa kila mmoja alikuwa na utambulisho wake. Zaidi ya hapo, eneo hilo lilizungukwa na kioo kinene kischopenya risasi ambacho kilikuwa kizuizi kati ya ilipo kokwa na walipo wageni. Hata hapa alipoingia Simbeye na wenzake palikuwa ni nje ya kile kioo. Kamera za usalama zilitegwa kila mahali. Kengele za hatari nazo zilifungwa kwa ustadi wa hali ya juu sana. Ungeingiaje humo ndani? Kila mmoja aliwaza.

“Ok! Sasa naomba kisiguswe chochote na wala eneo hili asiingie wala kukaribia yeyote mpaka amri nyingine itakapotolewa!” Simbeye aliwaeleza wanausalama waliokuwa pale na lisha akaelekea kwenye gari lake. Aliingia na kuketi kwenye kiti cha abiria. Dereva wake alipotaka kuwasha tayari kwa kuliondoa gari hilo, akamzuia kwanza. Macho yake yalikuwa yakitazama nyendo za wapita njia wa eneo lile mmoja baada ya mwingine. Kwa jicho lake la kikachero, hakuna kipya wala cha kuhofia alichokiona. “Twende” akamwambia dereva wake. Inspekta Simbeye aliliacha eneo lile majira ya saa nne na nusu asubuhi nakutokomea mjini. Akili na mawazo yake vyote vikadidimia kwenye kilindi cha fikra kuhusu tukio hilo lililotokea katika jengo la makumbusho ya Taifa. Hakuna chombo chochote cha habari kilichojua juu ya tukio hilo.

Itandelea...



Soma riwaya hii kupitia

www.kitabumarket.co.tz

HADITHI: TUHUMA (2)- Na: Shujaa Maneno

SURA YA I

Inspekta huyo kijana, akiwa ndani ya sare yake ya kipolisi aliachia tabasamu pana kwa lile alilolifanya. Akashusha bunduki yake nakuitua ardhini kisha mkono wake ukachomoa pakiti ya sigara na kutoa moja kisha kuibana kwa papi za midomo yake. Aliporudisha pakiti mfukoni, akachukua kiberiti cha gesi na kuiwasha. Alipiga pafu tatu za haraka na kisha akaichomoa na kuibana kwa vidole vyake akitazama kule ambako Sesko alitumbukia na gari lake...

Songa nayo...

Inspekta Kombo alibaki palepale, macho yake yalikaza kutazama msafara ule ambao sasa ulisimama na walio-mo kwenye magari yale kuteremka. Wengine waliokuwa na nguvu walikimbilia bondeni kule ambako gari la Bosi Sesko liliangukia. Waliamini kuwa, hata kama moto mkubwa unaendelea kuwaka bado wangeweza kufanya lolote kuokoa maisha ya Sesko Kavilondo.

Kutoka kule chini, Kombo alikuwa akisikia kelele na mayoe ya watu wakihimizana kufanya jambo fulani. Alibaki pale kuhakikisha mwisho wa yote ni nini. Ijapokuwa baridi kali lilikuwa likimnyanyasa, Kombo alipapa kuhakikisha kuwa ameimaliza safari ya Sesko.

Alinua mkono wake na kuitazama saa aina ya Solex aliyovaa. Saa zilikuwa zimeyoyoma kwelikweli. Akaiinua bunduki yake na kujitwika begani kisha akajinyanyua kutoka kweye lile jiwe alilotumia kulenga shabaha. Alivuta hatua na kupenyapenya katika vichaka vilivyofungamana mlimani hapo. Akafanikiwa kuifikia barabara kubwa ya vumbi iliyopita kwenye kijiji cha karibu.

Nina uhakika safari hii nimempata! Akawaza.

** ** *

Wale walioambatana na Sesko katika msafara ule walijitahidi kwa hali na mali kumuokoa bosu wao. Kila kili-chofaakutumiwa kuuzimamoto ule kilitumika. Wakafanikiwa! Wakati mimi na wewe tunapofurshia kufa kwa mbaya wetu basi wengine hutokwa machozi dhidi ya huyohuyo ambaye wewe umemwita mbaya.

Tofauti na mawazo ya Kombo, Sesko hakuwa amekufa bali alikuwa katika hali mbaya sana. hakuwa akiongea wala kutazama. Alikuwa kimya kabisa

huku damu zikimvuja kila panapostahili kuvuja. Huku na huko, vijana wake walifanikiwa kumnasua kwenye vyuma vigumu vya mjerumani vilivyo pande zote na kumsogezea kivuli cha kifo sentimite chache sana kutoka hapo alipo. Haraka haraka walimbeka mzobe mzobe na kupandisha naye mpaka kule walikoacha magari yao. Msafara ule ukageza njia na kurudi mji mdogo wa Kyela.

Sesko Kavilondo, aliajiriwa serikalini miaka kadhaa nyuma kabla ya kuamua kuachana na ajira hiyo na kujikita katika biashara. Biashara hizo alizozianza akiwa ndani ya ajira yake baada ya kufahamiana na wafanya-biashara na watu maarufu wamiliki wa makampuni mbalimbali ambayo kwayo alikuwa akigawa zabuni mbalimbali zilimsukuma katika uamuzi huo wa kucha kazi na kuendelea kufanya biashara hizo na watu hao akiwa nje ya utumishi.

Akiwa nje ya utumishi ndipo alipoanza kufanya biashara haramu na walewalio ndani ya mifumo ya serikali, mfano kununua vitu mbalimbali vya serikali vinavyopigwa mnada. Cha kushangaza tu ni kwamba baadhi ya vitu bado vilikuwa vipya katika hali yake lakini yeye aliuziwa kwa bei ya kutupwa kisha kuvuza ama nje ya nchi au humuhumu ndani kwa bei ghali.

Mara kadhaa, Sesko Kavilondo amehusishwa na biashara haramu ya utakatishaji fedha. Alikamatwa na kuwekwa ndani lakini aliachiwa huru katika mazingira ambayo watu walishindwa kujua imekuwaje. Lakini waliishia tu kusema kuwa *'kuna wakubwa nyuma yake'*. Na baada ya hapo maisha yaliendelea kama kawaida. Sesko Kavilondo alikuwa hashindwi kufungua mlango wowote ule wa serikali muda wowote anaotaka. Mhujumu uchumi! Serikali ilimjua, wauza sheria walikuwa marafiki zake, wagavi na wanunuzi walikuwa maswahiba zake. Kama ungemtaja Mtanzania mwenye makazi mengi katika nchi mbalimbali ulimwenguni basi huyu alikuwa kinara. Wapo waliosema kuwa alikuwa kama bomba la kupitisha machafu ya vigogo. Alimiliki asasi hewa, iliyopokea misaada mikubwa kutokan-je, ilioelekezewa pesa nyingi na serikali katika miradi mbalimbali ya maendeleo. Mengine ilifanyika kidogo na mengine haikuonekana kabisa.

Sesko Kavilondo alikuwa na pesa mpaka anashindwa kupumua sawasawa. Alikuwa mkwasi mpaka oksijeni haimtoshi. Hata akiandaa sherehe ya kuzaliwa mtoto akiandaa basi usishangae mawaziri wakafika kula

HADITHI: TUHUMA (2) – Na: Shujaa Maneno

keki. Alikuwa na ushawishi, alijua kuwatumia vigogo. Aliwawekea sawa mipango yao. Alimiliki kila chombo cha usalama kuanzia sungusungu wa mtaa wake mpaka makamanda wa vikosi nyeti.

Hospitali ya Kanda Mbeya ilimpokea Sesko Kavilondo akiwa hajitambui kabisa, yaani robo tatu na nusu robo mfu. Mwili wake ulikuwa na majeraha ya moto na majeraha ya ajali ile. macho yamefumba, pumzi inapatikana kwa taabu, mapigo ya moyo ya kutafuta. Mganga mfawidhi aliposikia tu kuwa mgonjwa huyo ni Sesko Kavilondo, alichanganyikiwa. Maana alijua kuwa sasa hapo atapokea viongozi na serikali yao. Aliona wazi anapaswa kutoa huduma ya kipekee ya uangalizi wa kiumbe huyo. Heri wengine wafe tu kwa huduma mbovu lakini kibopa huyu apone.

Alikuwa kwenye kinywaji huko Nzovwe wakatika anapokea taarifa hiyo. akiwa kwenye gari kuelekea hospitali ili kuweka sawa huduma za mtu huyo na kuwapanga watu wake, simu yake inaita akipewa taarifa na msaidizi wa mkuu wa wilaya kuwa mkuu huyo atakuwa pale ndani ya dakika kumi tu. *Kumekucha!* Akawaza.

Wakati akitua simu yake na kushusha pumzi, akifikiri kuhusu ugeni mgonjwa, simu yake ikaita tena. Alikuwa katibu wa wizara ya afya, akampa maelekezo kutoka kwa waziri nini cha kufanya kuhusu mgonjwa.

Hospitali ya Kanda Mbeya ilijawa hekaheka usiku huo, askari kanzu tayari walifika kwa kificho kusikiliza minong'ono ya watu kuhusu tukio hilo. Lakini pia kuweka usalama kwa viongozi ambao tayari walikuwa mbioni kufika kumjulia hali bwanenye huyo.

** ** *

Siku moja baadae, Inspekta Kombo aliwasili jijini Dar es salaam. Aliripoti katika kituo chake cha kazi kama kawaida na kuendelea na majukumu mengine.

Jina la Inspekta Kombo liliweka makazi katika vinywa vya Watanzania wengi. Alipendwa na kusifiwa mno. Isingepita juma hata moja kabla magazeti hayajamwandika. Wengi walimwita Mzalendo. Kiongozi wa kikosi maalum cha kuzuia uhalifu nchini. Alijua na alikuwa na mbinu za kupambana na wahalifu. Alifyekelea mbali vikundi vya ujambazi, alipambana na majambazi sugu na kuyafichua huko yaliko. Kombo alipenda sana kazi yake, na alikuwa amekamilika kwenye medani.

Pamoja na yote hayo Maulidi Kombo au Inspekta alikuwa mtu wa swala tano, aliyeshika uislamu kwelikweli. Ujasili wake, wakati mwingine ulimjengea uadui

na vigogo wa serikali kwa kuwa alivuruga mipango yao oву na kuficua siri zingine zisizotakiwa kuwa wazi kabla mhusika hajafa.

Inspekta Maulidi Kombo aliutikisa mtandao wa wahalifu walio ndani na nje ya serikali. Aliogopwa, lakini aliwindwa kila kona.

Aliingia katika ofisi yake na kuketi juuya kiti cha mbao, meza yake iliyo tupu aliikuta kama alivyoiacha. Kabati kuku la chuma lililofungwa kwa mpira wa manati kwenye matundu ya vitasa vyake ambavyo sasa havikujulikana vilipo. Humo ndimo alimohifadhi nyaraka zake nyeti. Mlango uligongwa kwa kurdarudia.

Jamani hata sijapumzika! Akawaza. “Ingia!” akaitikia.

Askari moja konstebo akajitoma ndani ya ofisi ile na kusimama kwa nidhamu ya kijeshi.

Nini kitaendelea? Usikose sehemu ya pili katika toleo lijalo.



KALAMU YANGU

MSALITI: riwaya inayouweka mgogoro wa Kongo kifasihi

Unapozitaja riwaya za kijasusi zenye usisimuzi wa ajabu usomapo kwa hapa Tanzania, huwezi aha kuzitaja zile za mfululizo wa Kamanda Amata.

Katika safu hii ya KALAMU YANGU, tutasikia machache kuhusu riwaya ya MSALITI. Huyu hapa mwandishi wa kazi hii...

MSALITI ni moja ya riwaya pendwa ya kijasusi inayouweka mgogoro wa Mashariki ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo katika simulizi bunifu ya kuisimua. Riwaya hii iliyoandikwa na Richard Mwambe, inakubeba nakuzamisha kifasihi ndani kabisa ya misitu mizito ya Kongo ya Mashariki. Yeye mwenyewe anatumia.

Ileweke kuwa ni kazi bunifu ya kifasihi, haielezi ukweli wowote wa mgogoro huo. Kitu pekee kinachoifanya riwaya hii ionekane kama ni mkasa wa kweli ni majina ya miji kama Goma, Kivu, Beni na mingine mingine.

MSALITI ni hadithi yangu ya 42 kuandika lakini ni kitabu cha nane kuchapa. Naweza kusema ni kitabu kilichopendwa sana na watu waliopata kukisoma lakini kwangu binafsi bado kinapata upinzani mkubwa sana kati yacho na Operesheni Kashmiri na Harufu ya Kifo. Kama ukianambia nichague kitabu bora nilichowahi kuchapa ningumu kwangu kusema kipi ni bora, si MSALITI wala vinginevyo. Ukweli ni kwamba vyote ni bora sana sana sana.

Wazo la kuandika riwaya ya MSALITI lilinijia siku moja nilipokuwa na mazungumzo na rafiki yangu mmoja hivi ambaye aliwahi kwenda Beni huko Kongo katika misheni ya kulinda amani. Yeye alinisimulia mikasa mingi sana aliyokumbana nayo huko kama mwanajeshi, alivoshuhudia watu wanavyouawa na kutendewa kinyume na haki za binadamu. Inatisha! Pia katika masimulizi yao hayo alinisimulia kuhusiana na wanajeshi wa kulinda amani kutoka huko Tanzania waliwahi kushambuliwa vikali,

kisha baadae wakajibu mapigo na kusambaratisha kambi za waasi. Hapa sasa nikapata swali na kujiuliza, je; haikuwa usaliti? Hapa mawazo yangu yaligota. Hata nilipoachana naye nikaanza kuuchimba na kuusoma huu mgogoro kutoka katika vyanzo mbalimbali.

Kwa bahati pia nina marafiki kadhaa wakongomani ambao wanatoka maeneo hayo, niliwahoji baadhi ya maswali na wakanieleza mengi sana. Katika haya yote ndipo nikafuma kisa cha MSALITI kwa kuchanganya maudhui na kuisuka vyema simulizi hii.

Wengi wa wasomaji wangu hujikuta wana maswali mengi ndani yao kuhusu mwandishi wa kazi hizi. Najua hilo! Mimi siyo askari wala sihusiki na suala lolote kuhusiana na usalama kwa ujumla. Ila huwa napenda sana kusoma masuala ya kiusalama. Naweza kusema kwamba navutiwa na masuala ya kijeshi, kipelelezi na vitu kama hivo. Labda kwa sababu nimelelewa sana na askarikatika utoto wangu. Hata hivyo nimepitisha utoto wangu katika mazingira ya kambi za askari. Macho yangu yalikuwa yakiona askari na bunduki zao, wakifanya mazoezi ya kivita, wakikimbia mchakamchaka, wakicheza *martial art* na mambo mengine ya kimedani. Haya yote yamechangia kwa mimi kuandika sana masuala ya kichunguzi na kipelelezi.

Jalada la kitabu hiki linabeba mtazamo wa kimapenzi, yaani ukiliangalia hivi haraka haraka utajua ni riwaya ya maenzi. Lakini ukichunguza sana utaona juu ya picha iliyopo


kuna mduarawa *scope* ya mdunguaji ambayo itakupa picha ya nini kipo ndani.

Jalada hili linawakilisha jicho la mdunguaji anayemchungulia mwanamke aliyejilaza kitandani huku kaweka bilauli yenye mvinyo pembeni ya kalio lake. Hii picha nilimuomba mmoja wa marafiki zangu mwanamitindo, akaniruhusu kuitumia.

Sasa huyo mdunguaji anayechungulia hapo ni wewe msomaji kwa sababu ndiye unayeona kinachoonekana.

Kwakweli wengi waliosoma MSALITI kupitia mirejesho yao wamependa sana jinsi nilivyochezana kalamu katika kisa kile, jinsi nilivyoteka hisia zao kuwatoa katika ulimwengu halisi na kuwaingiza katika misitu ya Kongo kifasihi. Lakini kiukweli, kama kuna hadithi niliyotumia muda mfupi sana kuiandika ndiyo hii. Sikuwa tayari hata kuichapa kitabu, lakini kuna mtu mmoja kila kukicha alinisumbua sana kuusu MSALITI kuwa kitabu. Basi ikawa.

Pia kama wengi walivyotaka kujua kama kuna sehemu ya pili ya MSALITI, napenda tu kuwaambia kuwa, ndiyo, kitabu cha pili kitakuja kukikamilisha kile cha kwanza. Labda hayoyatakuwa huko mbeleni. Ila kwa sasa kwanza wasome MSALITI waelewe na waelewe nini nimewaambia mule ndani.



Inatoka ukurasa wa 33

Kwa mtazamo wa mtafiti kufikia sasa, hii ndiyo miundo pekee ya kimsingi ya silabi katika Kiswahili na mingine inayozuliwa na makundi mengine ya wanaisimu ni sawa tu na miundo hii iliyoainishwa hapo kabla. Kwa mfano, wapo wanaisimu wanaoongeza muundo mwingine wa silabi unaohusisha konsonanti za nusu irabu ambao ni silabi ile moja tu. Hatuungi uainishi wa namna hiyo kwani unakosa uhalisia. Kwa misingi hiyo katika kazi hii, nusu irabu zinasalia kushughulikiwa bila ubaguzi wala machagu kama zilivyo konsonanti nyingine. Kutokana na uchunguzi wetu, ni wazi kuwa kadri lugha inavyozidi kupanuka kimsamiati ndivyo kunavyozidi kutokea maneno yenye miundo mipya ya silabi. Hebu tazama muundo wa maneno haya mkopo kutoka TATAKI (2018) #trekta# na #transfoma# vilevile neno staftahi.

Maneno haya yana muundo ufuatao:

#trekta#	→	trek\$ta	KKIK\$KI
#transfoma#	→	trans\$fo\$ma	KKIKK\$KIKI

Hitimisho

Marejeleo

Habwe, J. na Karanja, P. (2004). Misingi ya Sarufi. Nairobi: Phoenix Press.

Mgullu, R. S. (1999). Mtalaa wa Isimu. Nairobi: Longman.

Mwita, L. C. (2007). 'Prenasalization and the IPA', katika UCLA Working Papers in Phonetics. 106, 58-67. Kutoka <http://www.ku.ac.ke/schools/humanities/images/stories/2016/scholarship.pdf>.

Nchimbi, A. S. (1995). 'Je, Mang'ong'o ni Fonimu au si Fonimu katika Kiswahili Sanifu?' katika Baragumu, 25-39. Maseno: Chuo Kikuu cha Maseno.

Obuchi, S. M. na Mukhwana, A. (2010). Muundo wa Kiswahili. Ngazi na Vipengele. Nairobi: A~Frame Publishers.

Okal, B. O. (2013). Uhakiki wa fonimu na miundo ya silabi za Kiswahili. Kioo cha Lugha, 13, 103–104.

Wagabi, W. J. (2023). Changamoto katika ujifunzaji fonolojia arudhi ya Kiswahili katika shule za upili, gatuji la Homa Bay, Kenya (Tasnifu ya Uzamili isiyochapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

MAKALA MAALUM

Miundo ya Silabi za Kiswahili Sanifu

MAKALA hii maalum inayoelekeza Miundo ya Silabi za Kiswahili Sanifu imeongezwa katika jarida letu kama chachu katika ukuzaji wa Kiswahili hususani kwa waandishi wa kazi za Kifasihi na Lugha kwa ujumla. Makala hii iliyosheheni umahiri katika ufafanuzi wa Miundo ya Silabi imetayarishwa na Wanga Wagabi

Ikisiri

Makala hii inachambua miundo ya

silabi za Kiswahili Sanifu

kwa kuzingatia tafsiri na

mitazamo ya wanaisimu

mbalimbali kuhusu idadi

na aina za silabi zinazojitokeza

katika lugha hii. Utafiti huu unaonyesha

kuwa ingawa Kiswahili kina

mfumo wa silabi tawala

unaofanana na ule wa

lugha nyingi duniani, kuna utofauti

mkubwa katika uainishaji wa miundo

hiyo, ambapo watafiti mbalimbali walibainisha idadi

tofauti za miundo ya silabi kuanzia mitano hadi kumi

na moja.

Kupitia uchambuzi wa mifano halisi ya miundo ya silabi

kama I, KI, K, KKI, KKII, KII, KKII, KIK, na

IK, makala hii inabainisha kuwa upanuzi wa msamiati

wa Kiswahili umechangia kuibuka kwa miundo mipya

ya silabi, hasa kutokana na maneno ya mkopo. Utafiti

huu unahitimisha kuwa utofauti wa miundo ya silabi

unatokana na upanuzi wa msamiati kupitia utohozi na

fasiri tofauti za wanaisimu kuhusu uhusiano wa fonimu

na silabi katika Kiswahili.

Silabi za Kiswahili Sanifu

Kiswahili kama zilivyo lugha nyinginezo huwa na mfumo

wa silabi tawala ambao vilevile hutokea katika lugha

nyingi ulimwenguni. Japo Kiswahili huwa na muundo

huo wa silabi pendwa pia huhusisha miundo mingine

tofauti ambayo hutazamwa kwa namna tofauti na wataalam

mbalimbali ambao wamewahi kujishughulisha na ufafanuzi wake.

Hali hii imesababisha kuwapo kwa idadi tofauti za miundo

hiyo ya silabi katika Kiswahili. Baadhi ya wanaisimu hawa ni

kama wafuatao; Obuchi na Mukhwana (2010), wanabainisha

miundo minane (8) ya silabi, Mwita (2009) anabainisha

miundo mitano ya silabi (5), Habwe na Karanja (2004) nao

waainisha miundo sita (6), naye Mgullu (1999) akifafanua

kuhusu miundo

**WANGA
WAGABI**



saba (7) ya silabi za Kiswahili. Wagabi

(2023) alitambua kuwa silabi za Kiswahili

zinatiwa katika makundi tisa

maarufu (9) na miundo mingine miwili

ambayo sio maarufu. Jumla ni miundo

kumi na moja (11) ya silabi.

Katika kazi hii tulizingatia maoni ya

Okal (2015) anayesema kuwa sauti

anazotaja Batibo kuwa ni fonimu

ng'ong'o kama vile /m, n/ pamoja na /

ny, ng', n, ng, nd/ kuwa zote ni fonimu

zinazojitegemea. Kwa hivyo, sauti

ng'ong'o hasa zenye herufi mbili

(tunazojiita vinazalishwa) zinafaa kuwakilishwa kwa

alama moja ya kifonetiki kama tunavyoona baina ya /

th, dh, gh, sh, ch/ zenye alama maalum. Alama hizo

tayari zinadokezwa na Mwita (2007: 65) kama vile /

nd, mb, ng na nj/ au tunaweza kutumia alama saidizi

kama vile /nd/, ng, n/ kifonolojia.

Miundo ya silabi za Kiswahili

Hapa miundo tisa ya silabi katika Kiswahili iliangaziwa

kama ifuatavyo:

a) Muundo wa Irabu pekee (I) - oa, au, ua.

Kuna maneno katika Kiswahili ambayo huundwa kwa

irabu pekee ambayo hujisimamia kama pigo kimatamshi.

Aghalabu vokali hizi huwa zinaambatana bila

kuunganishwa na konsonanti. Mifano ifuatayo

inaonyesha muundo huu:

(i) /o\$na/ (I\$KI)

(ii) /u\$za/ (I\$KI)

(iii) /a\$pa/ (I\$KI)

b) Muundo wa Konsonanti na Irabu (KI)

Huu ndio muundo ujitokezao sana katika lugha za

kibantu na katika lugha nyinginezo ulimwenguni. Silabi

katika muundo huu huanza kwa konsonanti ikifuatwa

na irabu. Mathalan katika maneno yafuatayo: kalamu,

darasa, vitabu, matata n.k

(i) /fa\$nya/ (KI\$KI)

MAKALA MAALUM

- (ii) /mbo\$na/ (KI\$KI)
(iii) /ka\$la\$mu/ (KI\$KI\$KI)

c) Muundo wa Konsonanti pekee (K)

Maneno yenye muundo huu katika Kiswahili kwa kawaida huwa sio mengi ijapokuwa huwepo baadhi ya maneno yanayoundwa na silabi za kinasali zinazohusisha konsonanti /n/ na /m/ zitumikazo kwenye mianzo. Maneno yafuatayo ndiyo yaonyeshayo muundo huu:

- (i) m\$me = Mme
(ii) m\$vi = Mvi
(iii) m\$to = Mto
(iv) n\$ta = Nta
(v) n\$zi = Nzi
(vi) n\$je = Nje
(vii) n\$ge = Nge - mdudu

Nasali hizo hupoteza usilabi zinapotokea kati au mwishoni mwa maneno.

d) Muundo wa mwambatano wa konsonanti mbili zikifuatwa na irabu (KKI)

Huu huwa muundo ambao huanza kwenye konsonanti mbili zikifuatwa nayo irabu. Konsonanti inayochukua nafasi ya pili inakuwa hasa kiyeyusho. Mifano ni kama ifuatayo;

- (i) /kwe\$nda/ (KKI\$KI)
(ii) /mbwe\$ha/ (KKI\$KI)
(iii) /bwe\$ni/ (KKI\$KI)

Mifano zaidi ni kama ifuatayo:

- (i) /pwa\$ni/ (KKI\$KI)
(ii) /mwe\$ndo/ (KKI\$KI)
(iii) /m\$chwa/ (K\$KKI)
(iv) /go\$ngwa/ (KI\$KKI)
(v) /ku\$mbwa/ (KI\$KKI)
(vi) /mbwe\$ha/ (KKI \$KI)
(vii) /spi\$ka/ (KKI \$KI)
(viii) /ske\$ti/ (KKI \$KI)
(ix) /shta\$ka/ (KKI \$KI)
(x) /bla\$nje\$ti/ (KKI \$KKI\$KI)

e) Muundo wa mwambatano wa konsonanti tatu na irabu (KKKI)

Muundo huu wa silabi hauna mifano mingi katika Kiswahili. Aidha, muundo wa aina hii hujitokeza hasa katika maneno ambayo yamekopwa jinsi tu ilivyo kwenye muundo wa silabi fungu; maneno haya yamefanyiwa utohozi kutoka lugha nyingine za kigeni. Tazama mifano ifuatayo;

- (i) /skru\$bu/ (KKKI \$KI)
(ii) /spri\$ng'i/ (KKKI\$ KKI)
(iii) /stro\$be\$ri/ (KKKI\$ KI\$KI)

f) Muundo wa KII

Muundo huu hujitokeza katika maneno yaliyo na mifuatano ya irabu mbili zinazofanana.

/njaa/ → \$njaa\$: \$KII\$

Mifano zaidi ni kama vile, /saa/, /taa/, /jaa/, /kaa/, /tii/, /vaa/, /zaa/ n.k

g) Muundo wa KKII

Muundo huu ulitambuliwa katika mifano michache ifuatayo:

- (i) /staafu/ → \$ s t a a \$ f u : \$KKII\$KI
(ii) /staajabu/ → \$staa\$ja\$bu : \$KKII\$KI\$KI
(iii) /mstaarabu/ → \$m\$staa\$ra\$bu : \$K\$KKII\$KI\$KI

Muundo huu hutokea katika minyambuo ya maneno haya na katika uambishaji wa unominishaji wa maneno haya.

h) Muundo ya silabi fungu huwa na muundo wa KIKama IK

Muundo hii huwa na ruwaza mbili ambazo huweza kuwa KIK au IK.

1) Muundo wa KIK.

Silabi zenye muundo huu huwa zina konsonanti katika mwisho wake na utamkaji wake hukatika ghafla. Silabi huonekana imefungwa na konsonanti ambayo huwa imekaa kwenye mwisho wa silabi hiyo. Muundo huu hutokea kwenye maneno machache ambayo huwa yenye asili ya kigeni. Mathalan tazama silabi za kwanza katika maneno yafuatayo, mah-su-si, kib-la, kab-la, mas-ki-ni, bus-ta-ni, tan-bi-hi na daf-ta-ri.

- (i) #sentensi# → sen\$ten\$si: KIK \$ KIK \$ KI
(ii) #hamsini# → ham\$si\$ni : KIK \$ KI \$ KI
(iii) #labda# → lab\$da : KIK \$ KI
(iv) #maktaba# → mak\$ta\$ba : KIK \$ KI \$ KI

2) Muundo wa IK

- (i) #umma# → um\$ma : IK \$ KI
(ii) #alhamisi# → al\$ha\$mi\$si : I \$ KI\$KI\$KI
(iii) #ahsante# → ah\$san\$te : IK \$ KIK\$KI
- Mifano zaidi ni kama ifuatayo: ansari, ardhi, aprili, afkani, imla, ihsani, ihramu, inna, insafu, insha, inkishafi n.k. Tukitazama silabi kama vile 'lab' katika 'labda' au 'mak' katika 'maktaba'.

Inaendelea Ukurasa wa 30

WAANDISHI WAKUBWA WA FASIHI AFRIKA *inatoka ukurasa wa 8-9*

Mnamo mwaka 2003, alipokea Tuzo ya Nobel ya Fasihi.

Maandiko yake yanakagua kwa kina mamlaka, ukoloni, ukatili, maadili, na uwajibikaji wa binadamu.

Kwa nini yuko #7: Ufundi wa hali ya juu wa uandishi, ushawishi mkubwa duniani, tuzo kubwa, na kazi zilizoza mijadala ya kitaaluma na kifasihi kote duniani.

LAKINI HAPA NDIPO MPANGILIO UNAPOWEZA KUWA MGUMU...

Orodha ya 7 Bora haiwezi kuwabeba wote. Waandishi wengine wengi wa ajabu walizingatiwa kwa kina na walikaribia kuingia:

- * ASSIA DJEBAR
- * BEN OKRI
- * TAYEB SALIH
- * AHMADOU KOUROUMA
- * BESSIE HEAD
- * AMOS TUTUOLA
- * MARIAMA BÂ

Pia wapo waandishi wengine wa Afrika ambao wana sifa kamili za kuingia hapa.

Hivyo basi, orodha isichukuliwe kama thibitisho la kimahesabu kwamba mwandishi mmoja ni "bora" kuliko mwingine.

Lengo la orodha hii ni kuanzisha mjadala — sio kufunga mjadala.

Hapa kuna uchambuzi wa waandishi hawa wawili nguli kutoka Tanzania katika mtindo ule ule, ukiainisha mchango wao wa kipekee na nambari za alama kwa kuzingatia vigezo vile vile saba:

Kwa Tanzania kama orodha ingetupatia nafasi ya kuingiza waandishi wawili tungeingiza majina ya Sheikh Shaban Robert na Abdulrazak Gurnah.

8 — SHAABAN ROBERT | 95/100

Huyu ndiye "Shakespeare wa Fasihi ya Kiswahili na Tanzania." Shaaban Robert si mwandishi tu; ni baba wa fasihi ya Kiswahili ya kisasa na msingi wa lugha yenyewe.

Kazi zake kuu ni pamoja na Kusadikika, Kufikirika, Wasifu wa Siti Binti Saad, na Utengano.

Maandiko yake yalitofautishwa na uwezo mkubwa wa kifalsafa, maadili, matumizi ya ndani ya lugha, na ushairi uliotukuka. Alitumia fasihi kukosoa ukoloni, kuhamasisha usawa wa kijinsia, na kujenga misingi ya

utambulisho wa Mwafrika kabla hata nchi za Afrika hazijapata uhuru.

Kwa nini anastahili kuwepo: Yeye ndiye aliyetengeneza njia ya fasihi ya Lugha za Kiafrika. Bila Shaaban Robert, maendeleo ya fasihi ya Kiswahili katika Ukananda wa Afrika Mashariki yasingekuwa hapa yalipo leo. Legacy yake haina mwisho.


ABDULRAZAK GURNAH

Mwandishi wa riwaya mzaliwa wa Zanzibar ambaye kazi zake zimevuka mipaka ya dunia katika kuelezea athari za ukoloni na athari za ukimbizi.

Kazi zake kuu ni pamoja na Paradise, By the Sea, Afterlives, na Desertion.

Mnamo mwaka 2021, Abdulrazak Gurnah alihakikisha jina la Tanzania linaingia kwenye historia ya dunia kwa kushinda Tuzo ya Nobel ya Fasihi, akitambuliwa kwa usimulizi wake usio na ubaguzi wala upendeleo katika kuelezea athari za ukoloni na hatima ya wakimbizi kati ya utamaduni na mabara.

Kwa nini anastahili kuwepo: Ushindi wake wa Nobel, ufundi wa hali ya juu wa usimulizi wa kihistoria (Historical Fiction), na uwezo wake wa kuleta historia na utamaduni wa Pwani ya Afrika Mashariki na Bahari ya Hindi katika jukwaa kuu la kimataifa.



SHAABAN ROBERT
1909 –1962

jishindie

PILAU LA CHRISMAS

Je wajua?

Jarida la Ngurumo ya Mwandishi litatoa PILAU la Krismass kwa WATU WATATU tu watakaoshinda shindano dogo lifuatalo.

SHINDANO

Andika **INSHA** kuhusu **Jarida la Ngurumo ya Mwandishi**

- ♦ Maneno yasipungue 500 na yasizidi 750
- ♦ Font Size 12 — Times New Roman
- ♦ Nafasi kati ya Mistari ni 0.5
- ♦ Tuma document (MS Word) kama kiambatanisho kwenye Email: jamvilasimulizi@gmail.com
- ♦ Usiandike jina lako kwenye Document hiyo.
- ♦ Katika sehemu ya Email andika Jina lako kamili, na namba ya simu, na pahala unapoishi
- ♦ Mwisho wa kupokea ni Tarehe 5 Novemba 2026.

Washindi watatu watatangazwa kwenye Jarida la Ngurumo ya Mwandishi la Disemba 1. Na watapokea vifurushi vyao tarehe 20/12/2026

Kipande cha habari kitakachoshika nafasi ya kwanza kitachapishwa kwenye Jarida la Disemba 2026.

Vifurushi vya Pilau:

- 1 - Mshindi wa kwanza atapata kifurushi cha Pilau la Krismass cha Tsh 40,000,
- 2 - Mshindi wa PILI na wa TATU watapata kifurushi cha Pilau la Krismasi cha Tsh 30,000 kila mmoja.

Kuwa mmoja wa waundaji wa jarida hili...

Tutumie makala za kifasihi au za lugha ya Kiswahili, hadithi fupi, mashairi, matukio ya kifasihi na mambo mbalimbali ya kifasihi ili tuweze kuyachapisha katika jarida letu. Na kama unatoa kitabu kipya tujuze ili tukitangaze jaridani.

Jarida hili ni kwa ajiliyako mwandishi, msomaji na mlumbi wa Kiswahili. Karibu sana!



MEROME

COMPANY LIMITED

NI MABINGWA

wa kutengeneza



Karibuni sana!
wateja wetu



KWA MAWASILIANO ZAIDI:

+255 712 345 316



EMAIL:

meromecompany@gmail.com

www.richardmwambe.com
JAMVI
la **SIMULIZI**

Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi
kila baada ya miezi miwili
jamvilasimulizi@gmail.com